JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA KIDATO CHA NNE (CSEE) 2023

# ELIMU YA DINI YA KIISLAMU

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA KUHITIMU KIDATO CHA NNE (CSEE) 2023

# 015 ELIMU YA DINI YA KIISLAMU

*Kimechapishwa na*:
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P. 2624,
Dar es salaam, Tanzania.

**© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2024**

Haki zote zimehifadhiwa.

# YALIYOMO

DIBAJI ........................................................ iv

1.0 UTANGULIZI ........................................................ 1

2.0 TATHMINI YA KILA SWALI ........................................................ 3

2.1 SEHEMU A: Majibu ya Kuchagua na Kuoanisha ........................................................ 3
2.1.1 Swali la 1: Kuchagua Jibu Sahihi ........................................................ 3
2.1.2 Swali la 2: Nguzo za Uislamu ........................................................ 10
2.2 SEHEMU B: Majibu Mafupi ........................................................ 14
2.2.1 Swali la 3: Nguzo za Imani. ........................................................ 14
2.2.2 Swali la 4: Familia ya Kiislamu. ........................................................ 18
2.2.3 Swali la 5: Dola ya Kiislamu Madina. ........................................................ 22
2.2.4 Swali la 6: Mfumo wa Jamii ya Kiislamu. ........................................................ 26
2.2.5 Swali la 7: Haki na Uadilifu katika Uislamu. ........................................................ 30
2.2.6 Swali la 8: Historia ya Uislamu baada ya kutawafu Mtume (S.A.W).. 33
2.3 SEHEMU C: Maswali ya Insha ........................................................ 36
2.3.1 Swali la 9: Nguzo za Uislamu ........................................................ 36
2.3.2 Swali la 11: Sunnah na Hadithi. ........................................................ 41

3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU KWA KILA MADA ........................................................ 46

4.0 HITIMISHO ........................................................ 47

5.0 MAPENDEKEZO ........................................................ 47

Kiambatisho ........................................................ 48

Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa katika Mada CSEE 2023 ........................................................ 48

## DIBAJI

Taarifa hii ya Uchambuzi wa Majibu ya Watahiniwa katika Mtihani wa Kuhitimu Kidato cha Nne (CSEE) 2023 katika somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu imeandaliwa ili kutoa mrejesho kwa watahiniwa, walimu, wazazi, watunga sera na wadau wa elimu kwa ujumla kuhusu ufaulu wa watahiniwa katika somo hili. Katika taarifa hii uchambuzi umefanyika katika majibu ya watahiniwa kwa kuwa mtihani ni kiashiria kimojawapo kinachoonesha mambo ambayo watahiniwa hao waliweza kujifunza kwa usahihi na yale ambayo hawakuweza kujifunza katika kipindi cha miaka minne ya Elimu ya Sekondari.

Taarifa hii imeweka bayana jinsi ambavyo watahiniwa wameweza kupata alama za juu, wastani na za chini katika kila swali. Aidha, sampuli za majibu ya watahiniwa waliojibu vizuri na wale waliojibu vibaya zimeoneshwa. Vile vile, sababu mbalimbali zilizochangia baadhi ya watahiniwa kuweza kujibu maswali kwa usahihi zimeelezwa. Miongoni mwa sababu hizo ni pamoja na; kuelewa vema matakwa ya maswali na kuwa na maarifa ya kutosha juu ya mada mbalimbali za somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu. Aidha, uchambuzi umebaini kuwa watahiniwa walioshindwa kujibu maswali kwa usahihi walikosa maarifa katika baadhi ya mada za somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu na wengine walishindwa kubaini matakwa ya maswali. Uchambuzi umebaini pia udhaifu katika kujenga hoja katika kujibu maswali ya kujieleza kwa ufupi na yale ya insha.

Baraza la Mitihani la Tanzania lina imani kuwa mrejesho uliotolewa utawawezesha wadau wa elimu kuchukua hatua madhubuti za kuboresha mchakato wa ufundishaji, ujifunzaji na upimaji ili hatimaye kuondoa changamoto zilizoainishwa katika taarifa hii na hatimaye kuongeza kiwango cha ufaulu cha watahiniwa katika mitihani ijayo.

Baraza la Mitihani la Tanzania linatoa shukrani na pongezi za dhati kwa wote waliohusika katika kuandaa taarifa hii ya uchambuzi.

Dkt. Said Ally Mohamed
**KATIBU MTENDAJI**

# 1.0 UTANGULIZI

Taarifa hii ni matokeo ya uchambuzi wa majibu ya watahiniwa waliofanya Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Nne (CSEE) mwezi Novemba 2023 katika somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu. Mtihani huu uliandaliwa kwa kuzingatia muhtasari wa somo husika uliotolewa mwaka 2012 kwa Kidato cha I hadi IV.

Maswali yaliyotumika katika mtihani yaliandaliwa kutoka katika mada 15 kati ya ishirini (20) zilizopo katika muhtasari wa somo. Aidha, maswali hayo yaligawanywa katika sehemu tatu; A, B na C zenye jumla ya alama 100. Sehemu A ilikuwa na maswali mawili (1 na 2), sehemu B ilikuwa na maswali sita (3 hadi 8) na sehemu C ilikuwa na maswali matatu (09, 10 na 11). Mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote katika sehemu A, B na maswali mawili kutoka sehemu C.

Watahiniwa waliosajiliwa kufanya mtihani wa somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu mwaka 2023 walikuwa 83,763 kati yao watahiniwa 81,023 sawa na asilimia 96.73 walifanya mtihani. Idadi hiyo ya waliofanya mtihani inaonesha upungufu wa watahiniwa 3,207 ikilinganishwa na watahiniwa 84,230 waliofanya mtihani wa somo hili mwaka 2022. Aidha, kati ya watahiniwa 81,023 waliofanya mtihani mwaka 2023, watahiniwa 65,982 walifaulu katika madaraja mbalimbali. Jedwali lifuatalo linaonesha madaraja ya watahiniwa hao ikilinganishwa na mwaka 2022.

**Jedwali Na. 1: Ulinganifu wa Ufaulu kati ya Mwaka 2023 na 2022**

| Mwaka | % Ya Ufaulu | Madaraja | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | A | B | C | D | F |
| 2023 | 81.82 | 1,804 | 7,370 | 32,789 | 24,019 | 14,656 |
| 2022 | 49.06 | 41 | 506 | 11,641 | 28,842 | 42,597 |

Jedwali Na. 1 linaonesha ongezeko la kiwango cha ufaulu kwa asilimia 32.76 mwaka 2023 ikilinganishwa na kiwango kilichofikiwa mwaka 2022. Aidha, idadi ya watahiniwa waliopata daraja F imepungua kwa takribani mara tatu ya idadi iliyokuwa mwaka 2022.

Kuongezeka kwa kiwango cha ufaulu mwaka 2023 kumechangiwa na kukua kwa uelewa kuhusu dhana ya upimaji wa umahiri kwa wadau na kuakisi kuwepo kwa mabadiliko chanya katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo hili.

Taarifa hii imechambua majibu ya watahiniwa katika kila swali kwa kulinganisha matakwa ya swali husika na majibu yake na kile ambacho watahiniwa wamejibu. Aidha, sampuli za majibu ya watahiniwa zimeambatanishwa ili kuonesha namna watahiniwa walivyojibu maswali mbalimbali. Taarifa hii imebainisha changamoto zilizowakabili watahiniwa katika kujibu maswali ili zifanyiwe kazi. Pamoja na uchambuzi wa majibu ya watahiniwa, taarifa hii imebainisha ufaulu wa watahiniwa hao katika mada mbalimbali zilizopimwa. Madaraja ya ufaulu katika somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu yalikuwa kama ifuatavyo:

**Jedwali Na. 2: Madaraja ya Ufaulu Somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu**

| ALAMA | DARAJA | MAONI |
|---|---|---|
| 75 – 100 | A | Vizuri Zaidi |
| 65 – 74 | B | Vizuri Sana |
| 45 – 64 | C | Vizuri |
| 30 – 44 | D | Inaridhisha |
| 0 – 29 | F | Dhaifu |

Jedwali Na. 2 linaonesha kuwa daraja la juu la ufaulu katika somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu ni A na daraja la mwisho ni F. Pamoja na kuwepo kwa madaraja hayo matano ya ufaulu, taarifa hii itatumia madaraja matatu katika kuwasilisha ngazi za ufaulu ambayo ni: vizuri, wastani na dhaifu. Ufaulu utakuwa dhaifu ikiwa asilimia ya watahiniwa waliofaulu katika swali ni 0 hadi 29. Ufaulu utakuwa wa wastani ikiwa watahiniwa waliofaulu katika swali ni kati ya asilimia 30 hadi 64 na ufaulu utakuwa mzuri ikiwa asilimia ya watahiniwa waliofaulu katika swali hilo ni 65 hadi 100.

Aidha, hitimisho na mapendekezo kutokana na uchambuzi wa majibu ya watahiniwa umetolewa katika sehemu ya mwisho ya taarifa hii. Inatarajiwa kuwa matokeo ya uchambuzi huu yatatumika katika kuimarisha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu kwa wanafunzi na hatimaye kuboresha kiwango cha ufaulu katika mitihani ijayo.

## 2.0 TATHMINI YA KILA SWALI

Tathmini ya kila swali imefanyika kwa kubainisha alichotakiwa kufanya mtahiniwa kwa mujibu wa matakwa ya swali, umahiri uliokusudiwa katika swali au kipengele husika, kisha idadi ya watahiniwa waliojibu swali hilo na kiwango chao cha ufaulu katika kila swali.


## 2.1 SEHEMU A: Majibu ya Kuchagua na Kuoanisha

Sehemu hii ilikuwa na maswali mawili (1 na 2). Swali la kwanza lilikuwa la kuchagua jibu sahihi kutoka katika machaguo matano (A, B, C, D na E). Swali hilo lilikuwa na vipengele kumi (10) ambapo kila kimoja kilikuwa na alama 1, hivyo; swali zima lilikuwa na alama 10. Swali la pili lilikuwa la kuoanisha lenye vipengele sita (6) ambapo kila kimoja kilikuwa na alama 1, hivyo, swali zima lilikuwa na alama 6. Kwa ujumla sehemu hii ilikuwa na alama 16.

### 2.1.1 Swali la 1: Kuchagua Jibu Sahihi

Swali la 1 lilikuwa na vipengele kumi (i) - (x) kutoka katika mada za: *Mtazamo wa Uislamu juu ya Elimu, Imani ya Kiislamu, Mtazamo wa Uislamu juu ya Dini, Fiqh, Mambo ya Lazima Kufanyiwa Maiti Muislamu, Bara Arab zama za Jahiliyah karne ya 6 A.D, Historia katika Uislamu, Sunnah na Hadith, Qur'an na Nguzo za Uislamu.* Mtahiniwa alitakiwa kuchagua jibu sahihi kati ya machaguo matano aliyopewa (A, B, C, D na E) kisha kuandika herufi ya jibu hilo katika kijitabu chake cha kujibia.

Takwimu zinaonesha kuwa swali hili lilijibiwa na watahiniwa wote 81,023 waliofanya mtihani. Kati yao watahiniwa 50,402 (62.21%) walipata alama 3 hadi 6 ambao ni ufaulu wa wastani. Watahiniwa 21,974 (27.12%) walipata alama 3.5 hadi 6 ambao ni ufaulu mzuri na watahiniwa 8,647 (10.67%) walipata alama 0 hadi 2 ambao ni ufaulu dhaifu. Muhtasari wa ufaulu wa watahiniwa hao kwa asilimia ni kama unavyoonekana katika chati Na. 1.




**Chati Na. 1:** *Asilimia ya Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 1*

Chati Na. 1 inaonesha kuwa, ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri kwani asilimia 89.33 ya watahiniwa walipata alama 3 hadi 10 ikilinganishwa na asilimia 10.63 ya waliopata alama hafifu (0 hadi 2).

Ufaulu mzuri katika swali hili umechangiwa na watahiniwa kuwa na maarifa ya kutosha katika mada zilizounda vipengele mbalimbali vya swali na uwezo wao wa kubaini matakwa ya vipengele hivyo. Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika kila kipengele umefanyika kama ifuatavyo;

Katika kipengele cha (i); mtahiniwa alitakiwa kubaini jambo ambalo linazingatiwa katika Uislamu katika kufafanua maana ya Elimu. Kipengele hiki kilipima umahiri wa watahiniwa kuhusu dhana ya Elimu kwa mujibu wa mafundisho ya Uislamu. Watahiniwa walioelewa vema dhana hiyo walichagua jibu sahihi D *Ufanisi na ubora wa vitendo*, kwa kuwa katika Uislamu kipimo cha msingi cha Elimu ya mtu ni ufanisi wake katika kazi na vitendo au tabia njema.

Watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi katika kipengele hiki, baadhi yao walichagua vipotoshi A *Alama za ufaulu katika vyeti na C Aina ya ajira wanayoweza kupata*, Vipotoshi A na C havikuwa sahihi kwani hoja hizo hazitoshelezi dhana ya elimu, kwakuwa elimu halisi ni

yale yanayobaki baada ya nadharia za darasani na vyeti unavyomiliki. Wengine walichagua kipotoshi B *Uwezo wa kutambua mazingira.* Hoja hii haikuwa sahihi kwani dhana ya elimu kwa mujibu wa Uislamu inazingatia maendeleo kamilifu ya mwanadamu katika mahitaji yake yote ya kimwili, kihisia, kiakili, na kiroho. Hivyo, elimu ikimuwezesha mwanadamu kutambua mazingira pekee haitoshelezi kukamilisha maana yake. Wengine walichagua kipotoshi E *Uwezo wa kuchambua na kueleza.* Hoja hii pia haikuwa sahihi kwani maana ya elimu kwa mujibu wa Uislamu inabainika katika vitendo na sio maneno.

Kipengele cha (ii); mtahiniwa alitakiwa kubainisha itikadi ya Uislamu iliyoelezwa katika tafsiri ya Aya ya Qur'an inayosema, *"Haitokei msiba katika ardhi wala katika nafsi zenu ila umekwisha andikwa katika kitabu kabla hatujaumba. Kwa yakini hilo ni sahali kwa Allah"* Kipengele hiki kiliwapima watahiniwa umahiri wa kuchambua maneno ya Allah (S.W) ili kubaini itikadi ya Kiislamu iliyozungumziwa ndani yake. Jibu sahihi katika kipengele hiki lilikuwa herufi C *Qadar ya Allah (S.W),* kwani Aya hiyo ilibainisha wazi juu ya mpango wa Mwenyezi Mungu (S.W) kwa viumbe na uwezo wake.

Watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi walichagua herufi A, *Upweke wa Allah,* itikadi ambayo inajitokeza mara nyingi katika Aya zinazoeleza umoja wa Mwenyezi Mungu (S.W). B *Vitabu vya Allah,* Kitabu kilichotajwa kwenye Aya hiyo sio katika vitabu vya mwongozo ambavyo vimetajwa katika itikadi ya Uislamu bali ni kitabu cha kumbukumbu ya amali za mja. Kadhalika, waliochagua kipotoshi E *Malaika wa Allah (S.W)* na D *Mitume wa Allah* hawakuwa sahihi kwani ujumbe wa Aya husika haukutaja chochote kuhusu itikadi hizo. Kwa ujumla watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi katika kipotoshi hiki walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu nguzo za Imani ya Kiislamu na msisitizo wake katika Qur'an tukufu.

Katika kipengele cha (iii); mtahiniwa alitakiwa kubainisha mfumo wa maisha ambao umeathiri tabia na mwendo wa mtu ambaye anajizuia na vyakula vizuri, anavaa nguo chakavu na kuishi katika nyumba isiyo sakafiwa akiamini kuwa kufanya hivyo ni kujikurubisha zaidi kwa Mungu. Kipengele hiki kilipima umahiri wa watahiniwa kuchambua dhana ya Dini na athari zake katika maisha ya wafuasi wake. Watahiniwa mahiri katika aina mbalimbali za Dini walichagua jibu

sahihi E *Utawa.* Watahiniwa hao walielewa vema kwamba sifa zilizotajwa kwa muhtasari katika kipengele hiki zilitosha kueleza athari zinazoonekana wazi kwa wafuasi wa itikadi hiyo.

Aidha, watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi katika kipengele hiki kwa ujumla hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu aina za Dini na athari zake kwa wafuasi wake. Baadhi yao walichagua kipotoshi A *Uislamu.* Jibu hili sio sahihi kwa sababu itikadi ya Uislamu inapishana na athari zilizotajwa kwani Uislamu unasisitiza ustawi wa mtu binafsi na jamii kwa ujumla. Wengine walichagua vipotoshi B *Uyahudi* na C *ukristo* itikadi ambazo pia zinapishana na athari zilizotajwa kwani Dini hizo katika nyanja ya ustawi wa waumini wake ni kama ulivyo Uislamu. Kadhalika, waliochagua kipotoshi D *Umajusi* walioshindwa kuelewa kuwa taathira ya Umajusi ni katika ibada zao za kishirikina za kuabudu moto.

Kipengele cha (iv); mtahiniwa alitakiwa kubaini moja ya Ibada ambayo inaingia katika Fiqh-Muamalaat miongoni mwa Ibada alizopewa. Kipengele hiki kiliwapima watahiniwa umahiri wa kukumbuka Ibada mbalimbali na aina zake. Watahiniwa mahiri katika mada ya Fiqh waliweza kuchagua jibu sahihi B *Mirathi*, kwani walielewa kuwa Fiqh-Muamaalat ni mahususi katika ibada za kijamii mfano ndoa, talaka, Eda, mirathi na biashara.

Aidha, watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi kipengele hiki, hawakuweza kupambanua tofauti iliyopo kati ya Fiqh-Muamalat na Fiqh-Ibadaat. Hivyo, walichagua vipotoshi; A *Sala*, C *Zakka*, D *Funga* na E *Hijja* ambavyo vyote kwa ujumla vinaingia katika mifano ya Fiqh-Ibadaat ambayo inahusiana na matendo maalumu ya kiibada ambayo pia ni nguzo katika Uislamu.

Kipengele cha (v); mtahiniwa alitakiwa kubaini jambo ambalo ni lazima kutekelezwa katika mchakato wa kuosha maiti. Kipengele hiki kiliwapima watahiniwa umahiri wa kuelewa mambo muhimu katika mchakato wa kumuosha maiti. Jibu sahihi katika kipengele hiki lilikuwa A *Kumfunika shuka maiti gubigubi*, ambapo watahiniwa weledi katika mada ya Mambo ya lazima kufanyiwa Maiti wa Kiislamu waliweza kulichagua, ulazima wa jambo hilo unaambatana na heshima ya kustiriwa aliyonayo mwanadamu hata kama atakuwa maiti.

Watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi katika kipengele hiki, walichanganya baadhi ya mazoea ya kijamii na matendo ya Sunnah katika kumuosha maiti. Baadhi yao walichagua kipotoshi B *Kuanza na kumuweka Maiti udhu* kitendo ambacho hakihesabiwi katika ulazima bali ni Sunnah iliyosisitizwa. Kadhalika kipotoshi E *Kujizuia kuongea wakati wa kuosha* nalo ni katika orodha ya mambo ya Sunnah. Wengine walichagua kipotoshi C *Kutumia maji ya kisima au mto,* maji hayo yanaruhusiwa kutumiwa kwakuwa ni twahara hata hivyo si lazima kutumiwa aina hiyo ya maji katika mchakato wa kuosha maiti, hivyo maji ya aina nyingine pia inawezekana kutumika ilimradi ni twahara. Vile vile kipotoshi D *Kutumia kitanda kilichotobolewa,* hakuna ulazima wa kutumia aina mahususi ya kitanda kwani waoshaji wanaweza kutekeleza wajibu huo hata ikiwa bila kitanda kinachopaswa kuzingatiwa ni kumuosha katika sehemu yenye faragha na itakayorahisisha mchakato wa uoshaji.

Kipengele cha (vi); mtahiniwa alitakiwa kubaini sababu ya upinzani mkubwa wa Maquraysh kwa ujumbe wa Mtume Muhammad (S.A.W). Kipengele hiki kilipima umahiri wa mtahiniwa kuchambua historia ya juhudi za mwanzo za Mtume (S.A.W) akiwa Makkah. Watahiniwa mahiri katika historia ya Uislamu kipindi cha Makkah waliweza kujibu kwa usahihi kipengele hiki kwa kuchagua herufi A *Walihofia kuharibika kwa maslahi yao ya kimali* kwa kuwa walielewa vema kuwa Uislamu ungezuia njia zao za kuchuma mali kwa dhulma.

Watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi katika kipengele hicho walionesha kukosa maarifa juu ya historia ya Uislamu kipindi cha Makkah. Baadhi yao walichagua kipotoshi B *Waliogopa kuharibiwa kwa Makanisa yao,* hoja ambayo haikuwa sahihi kwa sababu Maquraysh hawakuwa Wakristo bali walikuwa washirikina walioabudu masanamu. Wengine walichagua kipotoshi C *Walihofia mustakbali wa miungu yao ya masanamu,* sababu hii ilikuwa ni njia ya kuficha au kulinda tabaka la watawala na wenye mali kwa watu wengi wa kawaida. Wengine walichagua vipotoshi D *Walihofia kupoteza ushawishi wa kuhudumia Qaaba* na E *Walihofia kufukuzwa katika mji mtakatifu wa Makka*. Majibu haya sio sahihi kwa sababu haukuwa mpango wa Mtume Muhammad (S.A.W) kumfukuza mtu yeyote katika mji wa Makka bali ilikuwa ni kuwalingania Uislamu. Ukweli huu ulithibiti baada ya Mtume (S.A.W) kuikomboa Makka na kuitawala, kwani hakumfukuza Mtu

yeyote wala hakumlazimisha yeyote kusilimu na hata ufunguo wa Al-Qaaba aliurudisha kwa kabila la Bani Abdi Dar kuendelea kushikilia licha ya kuwa baadhi yao bado walikuwa ni washirikina.

Kipengele cha (vii); mtahiniwa alitakiwa kubainisha Nabii aliyepokea majukumu ya ulinganiaji wa Dini ya Allah (S.W) baada ya Yaaqub (A.S). Kipengele hiki kilipima umahiri wa watahiniwa kukumbuka Manabii wa Allah (A.S) kwa mpangilio wa kuletwa duniani. Jibu sahihi katika kipengele hiki lilikuwa herufi C *Yusuf (A.S).* Aidha, watahiniwa waliojibu kwa usahihi kipengele hiki walionesha kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu historia ya Manabii wa Allah (S.W) na utaratibu wa kuletwa Duniani kutekeleza majukumu ya ulinganiaji wa Dini ya Allah (S.W).

Kwa upande mwingine, baadhi ya watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi walikosa maarifa ya kutosha kuhusu silsila ya kuletwa Mitume hapa ulimwenguni. Hivyo, walichagua vipotoshi A *Is-haq (A.S),* B *Mussa (A.S),* D *Il-yaas (A.S)* na E *Idrisa (A.S*). Majibu haya sio sahihi kwa sababu Mitume waliyoorodheshwa walikuja kabla yao (Nabii Idrisa (A.S) na Is-haq (A.S)) na Mitume wengine walikuja baada yao (Nabii Mussa (A.S) na Nabii Il-yaas (A.S)).

Kipengele cha (viii); mtahiniwa alitakiwa kubaini hoja inayothibitisha usahihi wa Hadithi kwa kuzingatia vigezo vya matini. Kipengele hiki kiliwapima watahiniwa umahiri wa kuchambua vigezo vya Hadithi sahihi katika matini (maneno yaliyomo katika simulizi). Jibu la swali hili lilikuwa herufi E *Kuwiana na mambo ya hakika,* ambapo watahiniwa waliojibu kwa usahihi walionesha kuelewa vema vigezo vya Hadithi sahihi ambavyo ni Isnad na Matini.

Aidha, watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi katika kipengele hiki, walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu sayansi ya Hadithi. Baadhi ya watahiniwa hao walichagua kipotoshi A *Wasimulizi wadhibitifu* na B *Wingi wa wasimulizi,* ambavyo si vigezo vya Matini bali ni vigezo vya Sanad (silsila ya wasimulizi). Wengine walichagua vipotoshi C *Kuandikwa na Bukhari* na D *Kuwepo kwenye vitabu sita,* ambavyo pia sio vigezo vya matin bali ni vigezo vya Rawi (waandishi wa Hadithi).


Kipengele cha (ix); mtahiniwa alitakiwa kubaini sababu isiyo sahihi katika tukio la kushushwa Qur'an kidogo kidogo. Kipengele hiki kiliwapima watahiniwa umahiri wa kuelewa historia ya Qur'an na namna ilivyoshushwa. Watahiniwa weledi waliitambua sababu hiyo ambayo ilikuwa katika herufi B *Kuwapa nafasi wengine kuleta mfano wake,* kwani hoja hiyo haikuwa sababu ya kushushwa Qur'an kidogo kidogo bali ilikuwa ni changamoto endelevu kwa watu wote wanaopinga kuwa Qur'an inatoka kwa Allah (S.W).

Aidha, watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi katika kipengele hiki, walikosa maarifa ya kutosha kuhusu historia ya Qur'an. Watahiniwa hao walichagua vipotoshi A *Kuuthibitisha moyo wa Mtume (S.A.W),* C *kufanya wepesi wa kufika ujumbe wake,* D *Waumini kupata wepesi wa kuihifadhi* na E *Kufanya wepesi katika utekelezaji wake.* Ambavyo vyote vilikuwa na sababu sahihi zinazobainisha kushuka kwa Qur'an kidogo kidogo. Hivyo ni wazi kuwa Kwa ujumla, watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu historia ya Qur'an.

Katika kipengele cha (x); mtahiniwa alitakiwa kubaini jambo ambalo linasisitizwa katika nguzo ya Shahada katika maisha ya Muumini. Kipengele hiki kiliwapima watahiniwa umahiri wa kuchambua nguzo ya kwanza ya Uislamu kivitendo. Watahiniwa mahiri katika nguzo hiyo walijibu kipengele hiki kwa kuchagua herufi E *Wajibu wa kumtii Allah (S.W) na Mtume (S.A.W).* Watahiniwa hao walielewa vema kuwa nguzo ya Shahada ni lango kuu la kujisalimisha na kujinyenyekeza kwa Mwenyezi Mungu (S.W) na Mtume wake (S.A.W) kwa maneno na vitendo katika safari yote ya maisha ya mwanadamu.


Watahiniwa walioshindwa katika kipengele hiki walionesha kukosa maarifa ya kutosha kuhusu nguzo ya Shahada. Baadhi yao walichagua kipotoshi A *Kufanya kazi za kutamkisha wengine,* ambalo halikuwa sahihi kwa sababu sio msisitizo uliopo katika nguzo ya Shahada. Wengine walichagua kipotoshi B *Kuanza jambo na jina la Allah (S.W) na Mtume (S.A.W),* ambalo pia halikuwa sahihi kwani msisitizo huo upo kwenye *Basmala* na sio Shahada. Kadhalika, waliochagua kipotoshi C *Hakuna Nabii mwingine isipokuwa Muhammad (S.A.W),* hawa hawakuelewa msisitizo wa Shahadah kwani kuambatana kwa Muhammad (S.A.W) ni ishara ya wasila wa utii kwa Mwenyezi Mungu (S.W) na haikuashiria lolote kuhusu mwisho wa utume. Wengine

walichagua kipotoshi D *Kutambua uwepo wa miungu wengi hapa duniani,* ni sahihi kuwa jambo hili linapatikana ndani ya Shahada, hata hivyo si jambo lililosisitizwa kwa muumini kuishi nalo bali msisitizo wake ni katika kukanusha miungu hiyo na kumtii Allah (S.W) pekee. Kielelezo Na. 1.1 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa katika swali hili.




Kielelezo Na. 1.1: Sampuli ya Majibu Sahihi ya Swali la 1

Kielelezo Na. 1.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu kwa usahihi katika swali hili.




Kielelezo Na. 1.2: Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi ya Swali la 1

### 2.1.2 Swali la 2: Nguzo za Uislamu

Swali hili lilitungwa kutoka mada ya Nguzo za Uislamu katika mada ndogo ya Kusimamisha Swala. Swali hili lilipima watahiniwa umahiri wa kuelewa nyakati za Sala. Aidha, mtahiniwa alitakiwa kuoanisha nyakati mahususi za Sala kulingana na mwenendo wa jua zilizotajwa katika orodha A (i) - (vi) na majina ya Sala zinazotekelezwa katika nyakati hizo katika orodha B (A) – (H) kisha kuandika herufi ya jibu sahihi kwa kila kipengele katika kijitabu chake cha kujibia.

Swali lilijibiwa na watahiniwa wote 81,023 waliofanya mtihani. Kati yao watahiniwa 34,291 (42.32%) walipata alama 4 hadi 6 ambao ni ufaulu mzuri na watahiniwa 31,176 (38.48%) walipata alama 2 na 3 ambao ni ufaulu wa wastani. Aidha, watahiniwa 15,556 (19.20%) walipata alama 0 na 1 ambao ni ufaulu dhaifu. Chati Na. 2. inaonesha muhtasari wa ufaulu wa watahiniwa hao kwa asilimia.




**Chati Na. 2:** *Asilimia ya Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 2*

Chati Na. 2 inaonesha kuwa ufaulu wa jumla katika swali hili ulikuwa mzuri kwani asilimia 80.80 ya watahiniwa walipata alama 2 hadi 6 ikilinganishwa na asilimia 19.20 ya watahiniwa waliopata alama 0 na 1.

Watahiniwa waliofaulu kwenye swali hili walionesha kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu Nyakati za Sala kwa kuzingatia mwenendo wa jua. Hivyo, waliweza kuoanisha kwa usahihi majira yaliyobainishwa katika Orodha A na majina ya Sala yaliyobainishwa katika Orodha B.

Katika kipengele cha (i); mtahiniwa alitakiwa kubaini sala inayoingia kuanzia urefu wa kivuli unapokuwa sawa na kitu halisi hadi kivuli kinapokuwa mara dufu ya urefu wa kitu halisi. Watahiniwa mahiri waliweza kubainisha jibu sahihi ambalo ni herufi C *Al-asr*. Watahiniwa hao walielewa vema athari ya kivuli cha jioni hadi pale jua linapokaribia kuzama upande wa Magharibi ambapo baina ya wakati huo ndipo Sala

ya Asr inatakiwa. Aidha, watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi, baadhi yao walichagua herufi F *Maghrib* ambalo halikuwa sahihi kwasababu Maghrib haipimwi kwa kivuli bali kuzama kwa jua na kujitokeza kwa mawingu mekundu. Wengine walichagua herufi *G Al-Ishaa*. Nao pia hawakuwa sahihi kwakuwa Ishaa ni wakati wa giza baada ya mawingu mekundu ya magharibi kutoweka.

Kipengele cha (ii); mtahiniwa alitakiwa kubaini sala inayotekelezwa kuanzia mawingu yanapobadilika na kuwa ya njano hadi usiku wa manane. Watahiniwa waliojibu vema kipengele hiki walichagua herufi G *Al-Ishaa.* Watahiniwa hao walielewa vizuri kuwa mabadiliko ya mawingu na kuwa ya njano ndio mwanzo wa giza pia walielewa kuwa Sala hii ndio pekee miongoni mwa Sala tano ambayo ina muda mrefu kati ya kuingia kwake hadi kuisha. Aidha, watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi baadhi yao walichagua herufi E *Al-fajr* jibu ambalo lipo mbali na wakati uliotajwa kwani Sala hii inaanza pale inapoonekana ishara ya weupe upande wa mashariki. Wengine walichagua *F Maghrib*, ambayo pia ilitofautiana sana na wakati uliotajwa kwani Maghrib ni sala yenye muda mfupi zaidi baina ya kuingia na kutoka kwake, kinyume na Sala ya Ishaa ambayo ndio jibu sahihi.


Katika kipengele cha (iii); mtahiniwa alitakiwa kubaini Sala inayotekelezwa baada ya jua kugeuka upande wa magharibi hadi pale urefu wa kivuli unapokuwa sawa na kitu halisi. Watahiniwa waliojibu kwa usahihi katika kipengele hiki walichagua herufi D *Dhuhur*, watahiniwa hao walielewa vema kuwa wakati uliotajwa unaingia mara tu baada ya kupita kwa wakati ulioharamishwa kusali (wakati ambao mtu anakikanyaga kivuli chake). Watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi baadhi yao walichagua herufi B *Istisqaa* ambayo si sahihi kwani *Istisqaa* ni Sala ambayo haina muda maalumu isipokuwa haitekelezwi katika nyakati zilizoharamishwa. Sala hiyo inaletwa ikiwa kuna hitajio la mvua (kuondosha ukame). Wengine walichagua herufi C *Al-asr,* ambayo si sahihi kwani Sala ya *Asr* inaanza mara baada ya kufanana urefu wa kivuli cha kitu halisi hadi kivuli hicho kitakapokuwa maradufu.

Katika kipengele cha (iv); mtahiniwa alitakiwa kubaini Sala inayotekelezwa kuanzia pale ambapo alama ya mstari mweupe inapojitokeza upande wa mashariki hadi mwangaza unapodhihiri. Watahiniwa weledi wa nyakati za Sala walichagua herufi E *Al-fajr*.

Watahiniwa hao walielewa vema kuwa muda wa kuingia na kutoka kwa Sala ya *Al-fajr* inaingia pale ishara ya mwangaza inapojitokeza upande wa mashariki. Aidha, watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi, baadhi yao walichagua herufi D *Dhuhr* ambalo ni kosa la wazi kwani *Dhuhr* ni mchana na wangine walichagua herufi H *Qusufi,* ambalo pia si sahihi kwani Sala hii inajitokeza wakati wa kupatwa kwa jua au mwezi. Kwa ujumla watahiniwa hao walikosa maarifa juu ya nyakati za Sala.

Kipengele cha (v); mtahiniwa alitakiwa kubaini Sala inayotekelezwa kuanzia jua linapozama hadi pale mawingu mekundu yanapobadilika na kuwa ya njano. Watahiniwa mahiri kuhusu nyakati za Sala walichagua jibu sahihi F *Maghrib,* wakati ambao ni mfupi sana kati ya nyakati tano za Sala za *Faradh.* Watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi, baadhi yao walichagua kipotoshi G *Al-Ishaa* Sala ambayo inaingia baada ya magharibi yaani kuanza kwa usiku. Wengine walioanisha na kipotoshi B *Istisqaa,* ambayo ni Sala ya kuomba mvua na haifungamani na wakati maalumu. Kwa ujumla katika swali hili watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi walionesha ukosefu wa maarifa ya kutosha na wengine kutokuwa na maarifa kabisa kuhusu nyakati za Sala.


Katika kipengele (vi); mtahiniwa alitakiwa kubaini Sala inayotekelezwa baada ya kuchomoza kwa jua kiasi cha mita tatu hadi kabla ya jua kufika kati kati. Watahiniwa weledi kuhusu nyakati za Sala walichagua jibu sahihi A *Dhuha,* Sala ambayo ni Sunnah muhimu aliyoifundisha Mtume (S.A.W). Aidha, watahiniwa waliokosa maarifa juu ya *Sunnah* hii baadhi yao walichagua herufi H *Qusufi,* ambayo ni Sala ya kupatwa kwa mwezi au jua. Wengine walichagua herufi E *Al-fajr* ambao walikosa maarifa na kuchanganya muda wa kuingia kwa Sala ya *Al-fajr* na wakati wa kuingia Sala ya *Dhuha* kwa kuwa nyakati hizo zinakaribiana. Kielelezo Na. 2.1 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa katika swali hili.



| 2 | ORODHA A | ORODHA B |
|---|---|---|
| | i | C |
| | ii | G |
| | iii | D |
| | iv | E |
| | v | F |
| | vi | A |

Kielelezo Na. 2.1: Sampuli ya Majibu Sahihi ya Swali la 2

Kielelezo Na. 2.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu kwa usahihi swali hili.


2 i → E
ii → F
iii → A
iv → C
v → D
vi → H

Kielelezo Na. 2.2: Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi ya Swali la 2


## 2.2 SEHEMU B: Majibu Mafupi

Sehemu hii ilikuwa na maswali sita ya majibu mafupi, kutoka mada za *Nguzo za Imani, Familia ya Kiislamu, Dola ya Kiislamu Madina, Mfumo wa jamii ya Kiislamu, Haki na Uadilifu na Historia ya Uislamu baada ya Kutawafu Mtume (S.A.W) hadi hivi leo.* Mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote. Kila swali lilikuwa na alama tisa (9), hivyo, jumla ya alama zote zilikuwa 54.

### 2.2.1 Swali la 3: Nguzo za Imani.

Katika swali hili mtahiniwa alitakiwa kubainisha tofauti sita baina ya Malaika na wanadamu. Swali hili lilipima umahiri wa watahiniwa kuchambua sifa mbalimbali zinazowatofautisha baina ya viumbe wanadamu na malaika.

Takwimu zinaonesha kuwa watahiniwa 81,023 (100%) walifanya swali hili, ambapo kati yao watahiniwa 50,066 (61.79%) walipata alama 6 hadi 9 ambao ni ufaulu mzuri. Watahiniwa 22,753 (28.08%) walipata alama 2.5 hadi 5.5 ambao ni ufaulu wa wastani na watahiniwa 8,204 (10.13%) walipata alama 0 hadi 2 ambao ni ufaulu dhaifu. Chati Na. 3 inaonesha muhtasari wa ufaulu wa watahiniwa hao kwa asilimia.





**Chati Na. 3:** *Asilimia ya Ufaulu wa Watahiniwa Katika Swali la 3*

Chati Na. 3 inaonesha hali ya ufaulu mzuri wa watahiniwa katika swali la 3 kwani asilimia 89.87 wamepata alama 2.5 hadi 9 ukilinganisha na asilimia 10.23 walio na ufaulu dhaifu.

Uchambuzi uliofanyika katika majibu ya watahiniwa waliofaulu umeonesha kuwa, watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu tofauti baina ya malaika na wanadamu. Aidha, katika majibu yao walieleza hoja mbalimbali zinazoonesha tofauti hizo kama vile: (i) *Malaika wameumbwa kutokana na nuru wakati wanadamu wameumbwa kwa udongo,* (ii) *Malaika hawana jinsia wakati wanadamu wanajinsia,* (iii) *Malaika ni viumbe wa kiroho wenye mbawa wakati wanadamu wameumbwa kwa maada bila ya mbawa,* (iv) *Malaika hawamuasi Allah (S.W) wakati wanadamu wanaweza kumuasi Allah (S.W),* (v) *Malaika hawana matashi ya kimwili kama vile kula, kulala, wakati wanadamu wana matashi ya kimwili na* (vi) *Malaika wanaweza kujimithilisha katika maumbile mbalimbali wakati wanadamu hawawezi kujibadili na kuwa kiumbe kingine kwa kiini macho* (vii) *Malaika hawaonekani katika maumbile yao ya asili (isipokuwa katika hali tatu, kwenye kutoa roho kwenye kutoa roho, siku ya kiama na peponi au motoni) wakati mwanadamu anaonekana, (viii) Malaika hawana hiyari kwa wanayoyafanya tofauti na wanadamu ambao wamepewa uchaguzi wa njia waitakayo,* (ix) *Malaika daraja lao halibadiliki tofauti na*

*wanadamu daraja lao linabadilika (wakifuata yale walioamrishwa Wanadamu wanakuwa na daraja bora zaidi kuliko Malaika) na wanapomuasi Allah (S.W) wanakuwa dhalili kuliko wanyama), (x) Malaika ni mtumishi wa Allah (S.W) lakini wanadamu ni makhalifa wa Allah (S.W)* (xi) *Malaika wana elimu ya kutekeleza kazi au majukumu yao maalumu waliopangiwa na Mwenyezi Mungu wakati wanadamu wana elimu pana katika nyanja mbalimbali na* (xii) *Malaika ni wengi wakati binaadamu ni wachache.* Kielelezo Na. 3.1 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa katika swali hili.



3. Tofauti sita kati ya Malaika na Binaadam.

| Malaika | Wanaadam |
|---|---|
| i. Wameumbwa kwa kutumia nuru | i. Wameumbwa kwa kutumia udongo. |
| ii. Ni viumbe wasio onekana kwa macho | ii. Ni viumbe wanao onekana kwa macho |
| iii. Ni viumbe wasio na matamanio wala jinsia | iii. Ni viumbe wenye matamanio na wenye jinsia |
| iv. Ni viumbe wanaotii maamrisho yote ya Allah (s.w). | iv. Ni viumbe wanaopinga baadhi ya maamrisho ya Allah (s.w). |
| v. Ni viumbe wasio kula wala kulala | v. Ni viumbe wanaokula na kulala |
| vi. Ni viumbe wenye mabawa | vi. Ni viumbe visivyo na mabawa. |


Kielelezo Na. 3.1: Sampuli ya Majibu Sahihi ya Swali la 3

Uchambuzi zaidi umeonesha kuwa watahiniwa waliopata alama za chini katika swali hili walikosa maarifa ya kutosha kuhusu tofauti baina ya Malaika na wanadamu na wengine walishindwa kubaini matakwa ya swali hilo. Sababu hizo zimejitokeza kutokana na aina ya majibu yaliyotolewa na watahiniwa hao katika kujibu swali hili.

Miongoni mwa watahiniwa walioonesha kukokosa maarifa kuhusu sifa zinazowatofautisha Malaika na wanadamu walitoa hoja kama vile: (i) *Malaika ameumbwa kwa ajili ya kumuabudu Allah (S.W) mpaka siku ya mwisho,* (ii) *Mwanadamu hafikii lengo la kuumbwa kwake,* (iii) *Malaika ameumbwa kwa umbile lililo bora (*iv) *Malaika ameumbwa ili afikie lengo la kuumbwa kwake wakati wanadamu ni tofauti, (v) Mwanadamu umbile lake ni la kidini wakati Malaika ni kiumbe kilicho hai.*

Wengine walieleza: (i) *Malaika ni viumbe walioumbwa na majukumu yao ili kuwafikishia Wanadamu wakati Wanadamu ni viumbe waliojaaliwa akili na ufahamu, (ii) Malaika ni viumbe walioletwa na Mwenyezi Mungu kuwatakia rehma viumbe wakati Wanadamu ni viumbe walioletwa kuja kumuabudu Allah na Mtume wake pamoja na Maswahaba zake. (iii) Malaika ni viumbe walioteremshiwa Wahyi lakini Mwanadamu ni mtu alieumbwa kutokana na udongo, (iv) Malaika wamepewa miujiza lakini Mwanadamu hawakupewa miujiza, (v) Malaika ni watumishi wa Allah lakini Wanadamu si watumishi wa Allah, (vi) Malaika wameumbwa kutokana na nuru lakini Wanadamu hawakuumbwa kutokana na nuru.* Wengine wameandika*: (i) Malaika ni waamnifu lakini Wanadamu si waminifu, (ii) Malaika ni viumbe walioumbwa na matashi ya Mwenyezi Mungu lakini wanadamu hawakuumbwa na matashi.*

Kadhalika, baadhi ya watahiniwa waliandika*; (i) Malaika wameumbwa kwa moto lakini mwanadamu ni kiumbe dhaifu, (ii) Malaika ni viumbe wanaoamrishwa lakini mwanadamu hawezi ukaamrishwa na mwenyewe Allah,(iii) Malaika hawana miguu lakini wanadamu wana miguu, (iv) Malaika wana Imani juu ya uwepo wa Allah lakini mwanadamu hana Imani, (v) Malaika ni kiumbe aliyeteuliwa na Allah (S.W) kwa ajili ya kufanya mema lakini wanadamu wameletwa duniani kwa ajili ya kukisoma kitabu kitukufu ambacho ni Qur'an na kusali na (vi) Malaika ni kiumbe aliyepewa uwezo wa kutambua mema na mabaya lakini wanadamu nao wamepewa uwezo mdogo wa kujua mema na mabaya.* Baadhi ya majibu haya yaliashiria kukosa maarifa ya kutosha kwa watahiniwa na wengine kushindwa kuelewa matakwa ya swali husika, hivyo; wakaandika hoja zisizo na mantiki. Kielelezo Na. 3.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu kwa usahihi katika swali hili.



SEHEMU B

3 (i) Malaika ameumbwa kwa ajili ya kuabudu Allah mpaka siku ya mwisho.

(ii) Mwanadamu hafikii lengo la kuumbwa kwake.

(iii) Mwanadamu ameumbwa kwa udongo.

(iv) Mwanadamu ameumbwa kwa ajili ya kumuabudu Allah.

(v) Malaika ameumbwa kwa umbo lililobora

(vi) Malaika ameumbwa ili afikie lengo la kuumbwa kwake.


Kielelezo Na. 3.1: Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi katika Swali la 3

Katika kielelezo Na 3.1 mtahiniwa ametoa hoja ambazo hazioneshi tofauti baina ya mwanadamu na malaika bali baadhi ya hoja hizo ni sifa zinazofanana na zingine ni sifa za kipekee za mwanadamu au malaika.

### 2.2.2 Swali la 4: Familia ya Kiislamu.

Swali la nne lilikuwa na vipengele viwili (a) na (b), kutoka katika mada ndogo ya *Ndoa katika Uislamu* na *Talaka na Eda*. Katika kipengele 4 (a) mtahiniwa alitakiwa kubainisha udhaifu wa madai kuwa Mahari yanashusha hadhi ya mwanamke kwa kutumia hoja tatu. Kadhalika, katika kipengele 4 (b) mtahiniwa alitakiwa kutoa sababu tatu za mwanamke wa Kiislamu aliyefiwa na mumewe kukaa Eda. Swali hili lilipima umahiri wa watahiniwa kuchambua dhana ya Mahari na Eda katika sharia ya Kiislamu.


Takwimu zinaonesha kuwa watahiniwa wote 81,023 (100%) walifanya swali hili. Kati yao, watahiniwa 35,975 (44.40%) walipata 0 hadi 2 ambao ni ufaulu dhaifu. Watahiniwa 35,901 (44.31%) walipata alama 2.5 hadi 5.5 ambao ni ufaulu wa wastani na watahiniwa 9,147 (11.29%) walipata alama 6 hadi 9 ambao ni ufaulu mzuri. Muhtasari wa ufaulu wa watahiniwa hao ni kama unavyoonekana katika Chati Na. 4.




**Chati Na. 4:** *Asilimia ya Ufaulu wa Watahiniwa Katika Swali la 4*


Chati Na. 4 inaonesha kuwa, ufaulu wa jumla katika swali hili ulikuwa wa wastani kwani asilimia 55.60 ya watahiniwa walipata alama 2.5 hadi 9 ikilinganishwa na asilimia 44.40 waliopata ufaulu dhaifu.

Watahiniwa waliofaulu katika kipengele cha 4 (a) walionesha kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu Ndoa ya Kiislamu na walielewa vema matakwa ya swali. Hivyo, waliweza kutumia maarifa yao vizuri na kujibu kama ifuatavyo; (*i*) *Mahari ni zawadi ya mwanamke ambayo anastahili kupewa na mume anaetaka kumuoa, (ii) Mahari ni ishara ya heshima ya utu wa mwanamke na (iii) Mahari sio bei ya kumnunua mwanamke kama inavyotazamwa na wasiokuwa Waislamu bali ni haki yake kutoka kwa Allah (S.W) aliyeamrisha wanaume kuwapa mahari wanawake wanaotaka kuwaoa.* Kielelezo Na. 4.1 (a) kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa katika swali hili.


4 a) i) Mahari ni zawadi ya mwanamke
ii) Mahari ni ishara au heshima ana yopewa mwanamke
iii) Mahari ni sheria ya dini ya uislamu


Kielelezo Na. 4.1 Sampuli ya Majibu Sahihi Katika Swali la 4 (a)

Katika kipengele cha 4 (b) Watahiniwa hao walibainisha sababu mbalimbali za kukaa Eda kama vile; (i) *Kumfanya mwanamke kuliwazika kutokana na msiba mkubwa uliompata,* (ii) *Kuangalia kama mwanamke ni mjamzito ili ajulikane baba wa mtoto na* (iii) *Kutii amri ya Allah (S.W) kwa kutaraji malipo mbele ya Haki*. Kielelezo Na. 4.2 (b) kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa katika swali hili.


b) → Eda ni sheria ya Uislamu
→ Eda kuepesha kuchanganya nasaba
→ Kuondoa machungu ya msiba

Kielelezo Na. 4.2 Sampuli ya Majibu Sahihi Katika Swali la 4 (b)


Uchambuzi zaidi uliofanyika katika majibu ya watahiniwa umeonesha kuwa, watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi katika swali hili walikosa maarifa ya kutosha katika mada ya Ndoa katika Uislamu. Vile vile, baadhi yao walishindwa kubaini matakwa ya swali, hali iliyosababisha watahiniwa hao kushindwa kujibu swali ipasavyo. Katika kipengele cha 4 (a) baadhi ya watahiniwa walioshindwa kuelewa matakwa ya swali walitoa hoja kama vile; *(i) Mwanamke atakuwa hana raha kwa ndoa yake kwa sababu muda wote atakuwa anasumbuliwa, (ii) Mwanamke atashushwa hadhi kwa mume na (iii) Mwanamke atakuwa sio mvumilivu na hatakuwa na subra na kwenye ndoa yake.* Mtahiniwa mwingine aliandika; (i) *Hawafuati mwenendo wa Mtume (S.A.W), (ii) Wanatoa maamuzi yasiyofaa kupitia nafsi zao,* (iii) *Hawajui na hawafahamu vema hadhi ya mwanamke katika Uislamu.* Vilevile, baadhi ya watahiniwa waliandika*; (i) Kwa mujibu wa sheria za Kiislamu mahari hayo yasingekuwa yanatolewa kama ingekuwa inashusha hadhi ya mwanamke, (ii) Jee aliyeamrisha mahari hayo kutolewa yeye alikuwa hajui hilo; hivyo alieamrisha kutoleana mahari ni kumshusha mwanamke hadhi yake hapo isingeliruhusiwa na (iii) Jee hakuna umuhimu wowote wa kutoleana mahari?* Majibu haya yaliashiria kuwa watahiniwa hao walishindwa kubaini matakwa ya swali, hivyo, walishindwa kutoa hoja muafaka kwa mujibu wa swali. Kielelezo Na. 4.3 (a) kinaonesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya mtahiniwa katika swali hili.


Q4. (a) i) Kwa mujibu wa sheria za Kiislamu -
mahari hayo yasingekuwa yanatolewa kama
ndio inashusha hadhi ya mwanamke
ii) Je aligeamrisha mahari hayo kutolewa
yeye alikuwa hajui hilo : hivyo aliamrisha -
kutoleana mahari kuwepo ni kumshusha -
mwanamke hadhi yake hapo isingeruhusiwa
iii) Je hakuna umuhimu wowote wa -
kutoleana Mahari? : kwa anayesema kuwa -
mahari inashusha hadhi ya mwanamke je -
umuhimu wake ni Upi wa kutoleana mahari

Kielelezo Na. 4.3 Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi Katika Swali la 4 (a)

Kadhalika, katika kipengele cha 4 (b) watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi baadhi yao walitoa hoja kama vile; *(i) Sababu moja wapo ni kwa ajili ya kutimiza muda wa kumlilia mumewe huyo huka eda pia kunamsaidia mwanamke awe karibu na mungu kwa ajili ya kumuombea mema. (ii) Humfanya mwanamke huyo aondokewe, na hali ya upweke katika maisha yake ya kipindi chote cha eda na (iii) Humfanya mwanamke huyo kuwa karibu na Allah (S.W) kwa kumtakia mema mumewe alietangulia mbele ya haki.* Mtahiniwa mwingine alijibu; (i) *Mwanamke kupata haki alizoachiwa na mumewe mfano mirathi.*

Wengine waliandika; (i) *Sababu watakuja waume kumposa hajamaliza eda yake,* (ii) *Kwa sababu eda hiyo yupo hukinga jasho la zinaa* na (iii) *Kwa sababu atachafua eda yake.* Majibu haya yalionesha kuwa watahiniwa hao hawakuelewa vema matakwa ya swali. Kielelezo Na. 4. (b) kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu kwa usahihi.


4 (b) (i) Sababu mojawapo ni kwa ajili ya kutimiza
muda wa kumlilia mumeo. huyo hukaa eda
pia kunamsaidia mwanamke huyo awe karibu
na mungu kwa ajili ya kumuombea mema.
ii) Kumfanya mwanamke huyo aondokewe -
na hali ya Upweke katika maisha yake
yote ya kipindi chote cha eda. hivyo anakuwa
kama amejisiti juu ya mambo mbali mbali
iii) Kumpanya mwanamke huyo kuwa -
karibu na Allah (s.w) kwa kumtakia mema
kwa mumeo aliyetangulia mbele ya haki.


Kielelezo Na. 4.2; Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi katika Swali la 4 (b)

Katika kielelezo namba 4.2 mtahiniwa alishindwa kutoa majibu sahihi yanayokidhi matakwa ya swali hili.

### 2.2.3 Swali la 5: Dola ya Kiislamu Madina.

Swali hili lilikuwa na kipengele viwili (a) na (b), kutoka katika mada ya *Dola ya Kiislamu Madina* ambapo katika kipengele cha 5 (a) mtahiniwa alitakiwa kutathmini faida tatu walizopata Waislamu baada ya matokeo ya vita ya Badr. Kipengele cha 5(b); mtahiniwa alitakiwa kulinganisha vitimbi vitatu vya wanafiki wa Madinah walivyomfanyia Mtume Muhammad (S.A.W) na vile wanavyofanyiwa Waislamu wa leo. Katika swali hili watahiniwa walipimwa umahiri wao katika kuchambua historia ya Uislamu kipindi cha Madinah na mafunzo mbalimbali yaliyopatikana kutoka katika uzoefu huo.


Takwimu zinaonesha kuwa watahiniwa 81,023 (100%) waliofanya mtihani walifanya swali hili. Kati yao watahiniwa 40,278 (49.71%) walipata alama 0 hadi 2 ambao ni ufaulu dhaifu. Watahiniwa 29,753 (36.72%) walipata alama 2.5 hadi 5.5 ambao ni ufaulu wa wastani na watahiniwa 10,992 (13.57%) walipata alama 6 hadi 9 ambao ni ufaulu mzuri. Chati Na. 5 inaonesha muhtasari wa ufaulu wa watahiniwa hao kwa asilimia.




**Chati Na. 5:** Asilimia ya Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 5


Chati Na. 5 inaonesha kuwa ufaulu wa watahiniwa katika swali ulikuwa wa wastani kwa kuwa asilimia 50.29 ya watahiniwa walipata alama 2.5 hadi 9.

Uchambuzi uliofanywa katika majibu ya watahiniwa waliojibu kwa usahihi katika kipengele cha 5 (a) ulibaini kuwa watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu historia ya Dola ya Kiislamu Madina na walielewa vema matakwa ya swali. Aidha, watahiniwa hao walibainisha faida tatu walizopata Waislamu baada ya matokeo ya vita vya *Badr* kama vile; (i) *Kuongezeka nguvu ya Uislamu na matumaini ya kusimamisha Uislamu pamoja na kuwepo kwa chuki za makafiri na washirikina, (ii) Kuonekana kwa nguvu ya Dola ya Kiislamu kwa kuweza kusimama dhidi ya maadui, (iii) Kudhihirika kwa ishara kuwa Uislamu ni Dini ya Allah (S.W).* Kielelezo Na. 5.1 (a) kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa katika swali hili.


a) ⇒ kuibuka na ushindi katika vita
⇒ Walipata msaada kutoka kwa
mwenyezimungu kwa kushushiwa na
malaika wao siku hiyo.
⇒ Walipata ngawira kama vile
farasi, ngamia na mali.

Kielelezo Na. 5.1: Sampuli ya Majibu Sahihi ya Swali la 5 (a).


Katika kipengele cha 5(b); watahiniwa hao waliweza kulinganisha vitimbi vya wanafiki wa Madina walivyomfanyia Mtume (S.A.W) na wanavyofanyiwa Waislamu wa leo ambapo walitoa hoja kama vile; (i) *Kutaka kumuua Mtume (S.A.W) na kuutokomeza Uislamu. Baadhi ya waislamu kushirikiana na maadui wa Uislamu kuuchafua Uislamu,* (ii) *wanafiki wakiongozwa na Abdala bin Ubayyi walichochea ugomvi baina ya Ansar na Muhajirina, baadhi ya Waislamu huchochea ugomvi baina ya Waislamu hususani katika tofauti za madhehebu* na (iii) *kumsaliti na kuvunja ahadi zao na Mtume (S.A.W) katika mikataba waliokubaliana mfano mkataba wa Hudaybiyya, baadhi ya Waislamu wanatumiwa na maadui wa Uislamu na kuwasaliti waislamu wenzao*. Kielelezo Na. 5.2 (b) kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa katika swali hili.


5(b)(iii) Kuwapa mateso makali waislamu. Enzi hizo
Wanafiki walikuwa wakiwapa mateso makali
Waislamu wa zama hizo kwa kuwapiga kuwapo
ra mali zao na wa leo kuwasusa na kuwatenga
Waislamu mfano China, Marekani na nchi nyingi
ne mbali mbali duniani

(iv) Kupinga Uislamu wanafiki walipinga -
Uislamu wakisema uislamu sio dini ya haki
Dini ya haki ni dini waliyoacha babu zetu.
Na wale ni kukataa ujumbe alioukuja nao
Mtume (s.a.w) ujumbe wa kuamrisha mema na
kukataza mabaya ila kwenye hii dunia -
Maovu yamezidi kina kirefu kuliko mema
Mfano liwati, wanawake kujiuza

Kielelezo Na. 5.2: Sampuli ya Majibu Sahihi ya Swali la 5 (b)

Uchambuzi zaidi uliofanyika katika majibu ya watahiniwa ulibaini kuwa, watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi swali la 5 (a) na (b) walikosa na maarifa ya kutosha kuhusu historia ya Dola ya Kiislamu Madina na wengine walishindwa kubaini matakwa ya swali. Miongoni mwao walitoa hoja kama vile: (i) *Waislamu kurudi Madina na Makka, (ii) Waislamu kuona jeshi pinzani ni wachache (iii) Waislamu kusamehewa na Allah.* Wengine walieleza (i) *Waislamu walipata kurejea Makka na kufanya Umrah kwa mara ya kwanza (ii) Waislamu walipata makafiri wakubwa wakubwa waliosilimu kwa mfano Walidi bin Walidi na Abuu Sufiyani.* Majibu hayo hayakuwa sahihi kwa sababu watahiniwa walichanganya umuhimu na faida za Mkataba wa Hudaibiyyah badala ya matokeo ya vita vya *Badr*. Hivyo, mtahiniwa hakuweza kupata alama. Kadhalika, mwingine aliandika; (iii) *Walitishia vita makabila yasiyo ishi baina ya Makka na Madina*, (ii) *Walitishia vita kwa watu wa kabila jengine* (iii*) Waliingia Madina kwa siri na kuingia navyo Makka*. Majibu hayo hayakuwa sahihi kwa sababu mtahiniwa alizungumzia njama za Makafiri dhidi ya Waislamu wa Makka badala ya matokeo ya vita vya *Badr*. Kielelezo Na. 5.3 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu kwa usahihi katika kipengele cha 5 (b).


5a) i) Waliomba msaada kwa allah (s.w)
ili wapate kushinda katika vita
yao maana hamna mungu
mwengine wa kuabudiwa isipokuwa
allah (s.w) peke yake na wakumu
omba.

ii) Walishinda vita kutokana na maqu
raysh kwasababu waao waliku
ja kuwapa vifaa fya kushindu
na katika vita yao.


iii) walileta silaha za kutosha baada ya
kuwauwa makafiri kwasababu maka
firi waliku wa hawataki kumuabudu
allah (s.w) kwahio walitumia nguvu
na adhabu yao nikuwauwa

Kielelezo Na. 5.3: Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi katika Swali la 5(a)

Katika kielelezo Na 5.3 mtahiniwa ametaja baadhi ya matukio yaliyojitokeza katika vita vya Badr badala ya kubainisha faida za matokeo ya vita hivyo.

Katika kipengele cha 5 (b); watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi walitaja matukio kama vile; (i) *Kuidharau Dini ya Mwenyezi Mungu, (ii) Kuvunja nyumba za Mwenyezi Mungu.* Watahiniwa wengine walijibu*; (i) Walimlaghai Mtume kutaka kumuua pamoja na Uislamu na Waislamu, (ii) Kutaka kuwaua waislamu katika vita hatimae kuwashinda maadui na (iii) Kutaka kuiporomosha Dola ya Mtume (S.A.W).* Matukio ambayo hayakujitokeza kwa wanafiki katika zama za Mtume (S.A.W) wala hayakuwa na uhusiano na sasa.

Watahiniwa ambao hawakuelewa matakwa ya kipengele hiki baadhi yao walitoa hoja kama vile; *(i) Kuendeleza Dola ya Kiislamu Madina, (ii) Kuchagua kiongozi aliyekuwa bora na (iii) Kukubaliana kiujumla kwa kumchagua kiongozi.* Hoja hizi ziliashiria kueleza mchango wa Masahaba (R.A) kinyume na matakwa ya swali katika kipengele husika. Kielelezo Na. 5.4 (b) kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu kwa usahihi.



5 (b) Vitimbi Vya wanafiki wa madina walivyo mfanyia Mtume Muhammad (S.A.W)
(i) Kutaka Kumuua wala hawa Kufanikiwa
(ii) Kumlenga mawe na Kumngowa jino
(iii) Kumchimbia shimo chini ya mlango wa nyumba yake
5 (b) Vitimbi Vya wanafiki wa madina wanavyo fanyiwa Waislamu wa leo.
(i) Kupigwa Kwa wale wasio Kuwa na hatia
(ii) Kuwaletea mavazi yaliyokuwa si ya maana (Kisheria)

Kielelezo Na. 5.2: Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi katika Swali la 5(b)

### 2.2.4 Swali la 6: Mfumo wa Jamii ya Kiislamu.

Swali hili lilikuwa na vipengele viwili (a) na (b) kutoka katika mada ya *Mfumo wa jamii ya Kiislamu* katika mada ndogo ya *Misingi ya Maadili katika Uislamu*. Katika kipengele cha 6(a) mtahiniwa alitakiwa kubainisha lengo la kuumbwa kwa Mwanadamu na katika kipengele cha 6(b); mtahiniwa alitakiwa kutumia hoja mbili kuonesha tofauti kati ya Mwanadamu na mnyama. Katika swali hili mtahiniwa alipimwa umahiri wake wa kiuchambuzi kutoka katika kubainisha tofauti kati ya mwanadamu na mnyama akihusianisha maumbile na mifumo waliyowekewa na Mwenyezi Mungu (S.W).


Takwimu zinaonesha kuwa watahiniwa wote 81,023 (100%) walifanya swali hili. Kati yao watahiniwa 34,826 (42.98%) walipata alama 6 hadi 9 ambao ni ufaulu mzuri. Watahiniwa 30,091 (37.14%) walipata alama 2.5 hadi 5.5 ambao ni ufaulu wa wastani na watahiniwa 16,106 (19.88%) walipata 0 hadi 2 ambao ni ufaulu dhaifu. Chati Na. 6 inaonesha muhtasari wa ufaulu wa watahiniwa hao katika asilimia.




**Chati Na 6:** *Asilimia ya Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 6*


Chati Na. 6 inaonesha ufaulu mzuri wa watahiniwa katika swali kwa kuwa asilimia 80.12 walipata alama 2.5 hadi 9 ikilinganishwa na asilimia 19.88 ya watahiniwa waliopata ufaulu dhaifu.

Watahiniwa waliofaulu vizuri katika swali hili walionesha kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu misingi ya maadili kwa mujibu wa Uislamu na walielewa vema matakwa ya swali hivyo waliweza kubainisha lengo la kuumbwa kwa mwanadamu na kutoa hoja zinazotofautisha baina ya mwanadamu na mnyama. Katika kipengele cha 6(a), watahiniwa hao walibainisha vema lengo la kuumbwa kwa Mwanadamu kuwa; *Ni kumuabudu Allah (S.W) kwa kufuata yale aliyoamrisha na kuacha aliyoyakataza katika kila kipengele cha maisha yake ya kibinafsi na kijamii*. Kielelezo Na. 6.2 (a) kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa katika swali hili.


6(a) lengo la kuumbwa kwa Mwanadamu ni Kumuabudu Allah (s.w) pamoja na kuacha yale yote aliyoyakataza na kufanya yale yote aliyoyaamrisha

Kielelezo Na. 6.2: Sampuli ya Majibu Sahihi ya Swali la 6(a)

Aidha, katika kipengele cha 6(b); watahiniwa hao walionesha tofauti zilizopo baina ya Mwanadamu na mnyama kwa hoja bayana kama vile; *(i) Mwanadamu ni kiumbe mwenye akili lakini wanyama hawana akili, (ii) Mwanadamu ni kiumbe aliyeumbwa kwa lengo la kumuabudu Allah (S.W) lakini wanyama wameumbwa kwa lengo la kumtumikia mwanadamu, (iii) Mwanadamu amepewa uwezo wa kutafuta Elimu yenye kumuwezesha kuendesha maisha yake hapa ulimwenguni kwa wepesi na kwa ufanisi lakini wanyama hawana uwezo wa kutafuta elimu, (iv) Mwanadamu ana uhuru wa kuchagua na kutenda alitakalo ndani ya kanuni za kimaumbile wakati wanyama hawana uwezo huo na (v) Binadamu ana maisha ya milele baada ya kufa wakati wanyama baada ya kuhukumiwa watageuka mchanga.* Kielelezo Na. 6.2 (b) kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa katika swali hili.



6 (b)(i) Mwanaadamu amepewa utambuzi akili
fikra pamoja na ujuzi wa kujua jambo -
zuri na baya lakini mnyama hajapewa -
utambuzi ~~fikra~~ fikra wala ujuzi wa kujua
mema na maovu kama ni kumuu mtu au -
kiumbe yeyote anaweza lakini mwanaadamu
yeye ana uwezo kujua maovu na machafu

(ii) Mwanaadamu anaweza kufanya makosa ya -
kumuasi Allah (s.w) Raqib na Atidy wakaandika
di makosa hayo lakini mnyama hafandi dhambi
kwa sababu hana uwezo wa kumuasi Allah (s.w)
Hajapewa fikra na utambuzi kama wa binadamu

Kielelezo Na. 6.2: Sampuli ya Majibu Sahihi ya Swali la 6 (b)

Kwa upande mwingine, watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi katika swali hili baadhi yao walishindwa kuelewa matakwa ya swali, na wengine hawakuwa na maarifa ya kutosha. Katika kipengele cha 6 (a), baadhi ya watahiniwa walioshindwa kubaini matakwa ya swali walichanganya majibu kwa kuandika hadhi ya Mwanadamu hapa ulimwenguni (khalifa) badala ya kubainisha lengo la kuumbwa kwa Mwanadamu ambalo ni kumuabudu Allah (S.W) katika kila kipengele cha maisha yake ya kibinafsi na kijamii. Vile vile watahiniwa wengine walichanganya lengo la Ibada ya Sala na lengo la kuumbwa Mwanadamu. Baadhi ya watahiniwa hao walitoa hoja kama vile; *Lengo la kuumbwa kwa mwanadamu ni kuwa Khalifa wa Allah (S.W) hapa*


*ulimwenguni.* Kielelezo Na. 6.3 (a) kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.


6(a) Lengo la kuumbwa mwanadamu ni kuwa halifa wa viumbe vyote duniani au ku wa kiongozi wa vyote viliyomo duniani

Kielelezo Na. 6.3: Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi Katika Swali la 6 (b)

Katika kipengele cha 6(b); baadhi ya watahiniwa hao walieleza kuwa; (i) *mwanadamu ametofautiana na mnyama ili kufanya ibada,* (ii) *Mwanadamu ni kiumbe ambae ameumbwa na miguu miwili na mikono miwili na mnyama ni kiumbe ambae ameumbwa na Allah kwa umbile lake la kinyama na ameumbwa kwa miguu minne.* Maelezo hayo yaliashiria kuwa watahiniwa walishindwa kubainini matakwa ya kipengele hicho hivyo, wakaeleza malengo ya tofauti baina ya wanyama na wanadamu.

Wengine waliandika; (i) *Mwanadamu katika kuishi kwake ni lazima apate pahala pazuri pa kula na kufanyia vitu vyengine lakini mnyama hana sehemu maalumu pa kula wala kupumzika,* (ii) *Mwanadamu habadiliki na kuwa mchanga wakati au siku ya kiama lakini mnyama anabadilika na kuwa mchanaga siku ya kiama na* (iii) *Mwanadamu kaumbwa na kuletwa duniani na Allah (S.W) na kuja kumlingania Mola wake ambae ndiye aliemleta duniani na mwisho wake wote.* Aidha, watahiniwa wengine waliandika; (i) *Mwanadamu anasuka mnyama hasuki,* (ii) *Binaadamu anasimama wima lakini myama hasimami wima na* (iii) *Mwanadamu anapika lakini myama hapiki.* Majibu ambayo yaliashiria kukosa maarifa ya kutosha katika mada iliyounda swali na kushindwa kuelewa matakwa ya kipengele husika. Kielelezo Na. 6.4 (b) kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.


6 Binadamu: Ni Kiumbe kilichoubwa na Allah S.w na Kinacho tembelea Miguu miwili(2) ila

7 Mnyama: Ni Kiumbe kilichoumbwa na Allah S.w na Kinachotembelea miguu minne(4)

Binadamu: Ni Kiumbe ambacho kikitaka kukidhi haja zake lazma kijifiche ila


ii Mnyama: Ni Kiumbe ambacho akitaka kukidhi haja zake hawezi akajificha.

Kielelezo Na. 6.1: Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi katika Swali la 6 (b)

### 2.2.5 Swali la 7: Haki na Uadilifu katika Uislamu.

Swali hili lilitoka katika mada ya *Haki na Uadilifu Katika Uislamu*, mada ndogo ya *Dhana ya Haki na Uadilifu katika Uislamu*. Katika swali hili mtahiniwa alitakiwa kufafanua mgawanyo wa haki za Mwenyezi Mungu (S.W) kwa mujibu wa Uislamu. Swali lilipima umahiri wa watahiniwa kuchambua mgawanyo wa haki za Mwenyezi Mungu (S.W) kwa mujibu wa mafundisho ya Uislamu.


Takwimu zinaonesha kuwa watahiniwa wote 81,023 (100%) waliofanya mtihani walijibu swali hili. Kati yao watahiniwa 48,668 (48.96%) walipata 0 hadi 2 ambao ni ufaulu dhaifu. Watahiniwa 25,243 (31.16%) walipata alama 2.5 hadi 5.5 ambao ni ufaulu wa wastani na watahiniwa 16,112 (19.88%) walipata alama 6 hadi 9 ambao ni ufaulu mzuri. Aidha, watahiniwa 31,857 kati ya watahiniwa waliokuwa na ufaulu hafifu walipata 0. Chati Na. 7 inaonesha muhtasari wa ufaulu wa watahiniwa hao kwa asilimia.




**Chati Na. 7:** *Asilimia ya Ufaulu wa Watahiniwa Katika Swali la 7*

Chati Na. 7 inaonesha kiwango cha wastani cha ufaulu katika swali hili kwa kuwa asilimia 51.04 ya watahiniwa walipata alama 2.5 hadi 9, ikilinganishwa na asilimia 48.96 waliopata ufaulu wa chini.

Watahiniwa waliofaulu katika swali hili walionesha kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu Haki za Mwenyezi Mungu (S.W) na walielewa vema matakwa ya swali hilo. Aidha, watahiniwa hao walifafanua mgawanyo wa Haki za Mwenyezi Mungu (S.W) kwa hoja mbili madhubuti ambazo ni; *(i) Haki ya Uungu; Mwenyezi Mungu (S.W) peke yake ndiye muumba wa vitu vyote na hakuna Mungu mwengine isipokuwa yeye Allah (S.W) hivyo anayo haki ya Uungu wake bila ya kushirikishwa na kitu chochote na (ii) Haki ya kuabudiwa; Allah (S.W) ndiye muumba, mlezi na mmiliki wa kila kitu*. Kielelezo Na 7.1 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa katika swali la 7.



7\. Haki za Mwenyezi Mungu ziko katika makundi yafuatayo -


(i) Haki ya Uungu Mwenyezi Mungu (s.w) peke yake ndiye muumba vitu vyote na hakuna Mungu mwengine isipokuwa yeye Allah (s.w) hivyo anayo haki ya Uungu wake bila kushirikishwa na chochote.

(ii) Haki ya kuabudiwa. Allah (s.w) anayo haki ya kuabudiwa kwani yeye ndie mwanzilishi wa ulimwengu huu na hauna oti daima hivyo tusipo mwabudu yeye tutamwabudu nani asiye andika? hivyo allah (s.w) anayo haki ya kuabudiwa kama aya ile iyosema katika surat Ikhlas aya ya 2.

Kielelezo Na. 7.1: Sampuli ya Majibu Sahihi ya Swali la 7

Watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi katika swali hili wengi walionesha kukosa maarifa ya kutosha kuhusu mgawanyo wa Haki za Mwenyezi Mungu. Miongoni mwao walitoa hoja kama vile; (i) *Haki ya kuwaheshimu wazazi, (ii) Haki ya kumfanyia wema mgeni na (iii) haki ya kumtendea wema jirani.* Wengine waliandika; *(i) Haki za raia katika Dola ya Kiislamu. (ii) Haki na mazingira ya mwanadamu*. Majibu haya hayakuwa sahihi kwani hayakueleza haki za Mwenyezi Mungu (S.W) bali yalitaja makundi mbalimbali ya haki kama vile haki za wazazi, haki za majirani na haki za raia katika Dola ya Kiislamu. Hivyo ni wazi kuwa watahiniwa hao walikosa maarifa ya kutosha kuhusu haki za Mwenyezi Mungu kwa mujibu wa Uislamu.

Baadhi ya watahiniwa walionesha kushindwa kuelewa matakwa ya swali na kutoa hoja kama vile; (i) *Haki ya Mwenyezi Mungu kuwapa wanadamu mazingira yenye kuvutia na (ii) Mwenyezi Mungu ana haki ya kuwapa wanadamu Elimu yenye muongozo.* Hoja hizo zinaeleza wajibu wa Mwenyezi Mungu kwa waja wake na sio haki zake Yeye kutoka kwa wanadamu. Kielelezo Na. 7.2 kinaonesha mfano wa majibu yasiyo sahihi ya mtahiniwa katika swali hili.


7 i Haki zinazofungamana baina ya mja na Muenyezi Mungu (SW).
Haki hizi huhusisha ibada zote ambazo mja anapaswa kuzifanya kwa ajili ya Mwenyezi Mungu (SW). Mfano ibada kama kufunga Ramadhani, kutoa zaka, kusimamisha swala na ibada nyengine.
7 ii Haki za Mwenyezi Mungu (SW) juu ya waja wa Mwenyezimungu (SW), au haki zinazofungamana baina ya mja juu ya waja wa Mwenyezi Mungu (SW).
Haki hizi mja huzitekeleza kwa kuwatekeleza waja wa mwenyezi mungu (SW).
Mfano:
Haki ya kuwaheshimu wazazi.
Haki ya kumfanyiwa wema ~~jirani~~ mgeni
Na haki ya kumtendea wema jirani

Kielelezo 7.2: Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi katika Swali la 7


Katika kielelezo Na. 7.2 mtahiniwa ameandika wajibu wa mwanadamu kwa Mwenyezi Mungu (S.W) na wanadamu wenzake badala ya kubainisha za haki za Mwenyezi Mungu (S.W) kutoka kwa waja wake.

### 2.2.6 Swali la 8: Historia ya Uislamu baada ya kutawafu Mtume (S.A.W)

Swali hili lilitoka katika mada ya *Historia ya Uislamu baada ya kutawafu Mtume (S.A.W) hadi hivi leo* katika mada ndogo ya *Ukuaji na Uendeshaji wa Dola ya Kiislamu wakati wa Makhalifa wanne waongofu*. Katika swali hili mtahiniwa alitakiwa kuchambua ishara tatu zilizowaongoza Waislamu kumchagua Abubakar (R.A) kuwa Khalifa wa kwanza baada ya kutawafu Mtume (S.A.W). Swali liliwapima watahiniwa umahiri wao katika kuchambua matukio muhimu yaliyowaashiria Maswahaba kumchagua Abubakar (R.A) kuwa kiongozi wa kwanza mapema baada ya kutawafu Mtume (S.A.W).

Takwimu zinaonesha kuwa watahiniwa 81,023 (100%) walijibu swali hili, ambapo kati yao watahiniwa 34,066 (42.05%) walipata alama 2.5 hadi 5.5 ambao ni ufaulu wa wastani. Watahiniwa 24,820 (30.63%) walipata alama 6 hadi 9 ambao ni ufaulu mzuri na watahiniwa 22,137


(27.32%) walipata 0 hadi 2 ambao ni ufaulu dhaifu. Chati Na. 8 inaonesha muhtasari wa ufaulu wa watahiniwa hao kwa asilimia.




**Chati Na.8:** *Asilimia ya Alama za Watahiniwa katika Swali la 8*

Chati Na. 8 inaonesha kuwa ufaulu wa jumla katika swali hili ulikuwa mzuri kwa kuwa asilimia 72.68 ya watahiniwa walipata alama 2.5 hadi 9 ikilinganishwa na asilimia 27.32 waliopata ufaulu dhaifu.

Uchambuzi uliofanywa katika majibu ya watahiniwa umeonesha kuwa Watahimiwa waliofaulu walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu historia ya ukuaji na uendeshaji wa Dola ya Kiislamu wakati wa Makhalifa waongofu, hivyo waliweza kubaini ishara mbalimbali zilizowaongoza Waislamu kumchagua Abubakar kuwa Khalifa wa kwanza. Miongoni mwa ishara walizotoa ni pamoja na; *(i) Ukaribu wake na Mtume (S.W) kuliko Swahaba mwingine yeyote, (ii) Alikuwa mtu mzima wa mwanzo mwanamme kuwa Muislamu, (iii) Alichaguliwa na Mtume (S.A.W) kuongoza Sala kipindi Mtume (S.A.W) ni mgonjwa. (iv) Alikuwa na sifa zote za kiongozi wa Kiislamu, (v) Alikuwa na umri mkubwa kuliko mtu yeyote katika ukumbi wa Thakifa Banu Saida.* Kielelezo Na. 8.1 kinaonesha mfano wa majibu sahihi ya mtahiniwa katika swali la 8.



8 Zifuatazo ni ishara tatu zilizowaongoza-
waislamu kumchagua Abubakar (R.A) kuwa -
khalifa wa kwanza baada ya kufawafu -
Mtume (s.a.w).
i) Alikuwa na sifa zote za kuwa Khalifa wa-
waislamu, mfano mjuzi wa Qur-an, Sunnah na-
mwenye tabia njema. Kutokana na Abubakar-
(r.a) kuwa na sifa zote zakuwa kiongozi mfa-
no mwenye tabia njema, mjuzi wa Qur-an, Su-
nnah ikawa ni ishara toska kwa waisla-
mu kumchagua khalifa Abubakar (r.a) kuwa-
ni khalifa wa kwanza baada ya -
kufawafu Mtume (s.a.w)

ii) Aliteuliwa na Mtume (s.a.w) kuongoza sala ya-
jamaa wakati Mtume alipokuwa Mgonjwa.
Vile vile kutokana na Mtume (s.a.w) kumchaga-
gua Abubakar (r.a) kuwaongoza waislamu ka-
tika sala ya jamaa wakati Mtume (s.a.w) ali-
pokuwa Mgonjwa ikawa ni ishara iliyowa-
fanya waislamu kumchagua Abubakar (r.a)-
kuwa khalifa wa kwanza baada ya kutawa-
fu Mtume (s.a.w).


iii) Alikuwa na Umri mkubwa na Mtumzima wa-
Mwanzo kuukubali Uislamu. Abubakar (r.a) ali-
kuwa ni Mtumzima wa mwanzo kuukubali-
Uislamu wakati Mtume (s.a.w) alipokuwa-
akilingania dini, kutokana na ishara hii-
ya kuwa Mtumzima wa mwanzo kuukubali
Uislamu na kumpenda kutoka moyoni ikapeleka
Abubakar kuwa khalifa wa kwanza wa Uislamu.

Kielelezo 8.1: Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 8

Uchambuzi zaidi uliofanyika katika majibu ya watahiniwa umeonesha kuwa, watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi katika swali hili hawakuwa na maarifa ya kutosha katika mada ya ukuaji na uendeshaji wa Dola ya Kiislamu wakati wa Makhalifa wanne waongofu na wengine walishindwa kubaini matakwa ya swali. Baadhi ya watahiniwa hao waliandika: (i) *Upendo wa khalifa Abubakar na ndugu zake*, (ii) *Mjomba ake Khalifa Abubakar aliwaendea vibaya majirani zake na kuwacheka.* (ii) *Matumizi mabaya ya fedha za serikali.* Mtahiniwa mwingine alieleza; (i) *Kuporomoka kwa Dola ya Kiislamu* (ii) *Yeye ndie alikuwa*

*akiwapa baia watu baada ya kutawafu Mtume (S.A.W) na* (iii) *Yeye ndie aliekuwa akiwasomesha watu masuala yanayohusu dini ya Kiislamu baada ya kutawafu Mtume (S.A.W).* Majibu hayo ya watahiniwa hayakuwa sahihi kwa mujibu wa swali husika, jambo linaloashiria kuwa hawakuwa na maarifa kuhusu historia ya Makhalifa waongofu.

Aidha, watahiniwa wengine walichanganya njia zilizotumika kuwapata viongozi wakati wa Makhalifa wanne waongofu na sababu za Abubakar kuchaguliwa kuwa Khalifa wa kwanza baada ya kutawafu Mtume (S.A.W) kama vile*;* (i) *Kuchaguliwa na viongozi, (ii) Kuchaguliwa kwa kupigiwa kura*. Hoja hizi ziliashiria kuwa watahiniwa hao walishindwa kubaini matakwa ya swali. Kielelezo Na. 8.2 kinaonesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya mtahiniwa katika swali la 8.


8 - Upendo wa Khalifa Abubakar na ndugu zake
- Mjomba wake Khalifa Abubakar aliwaidoya vile
ya majirani zake na kuwacha Ka.
- Mali nyingi mabaya yapesa za Serkali

Kielelezo 8.2 Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi katika Swali la 8

Katika Kielelezo Na. 8.2 mtahiniwa ameelezea uhusiano wa Khalifa Abubakar na ndugu pamoja na jirani zake kama ishara zilizowaongoza Waislamu kumchagua kuwa Khalifa wa kwanza sifa ambazo walikuwa nazo pia Maswahaba wengine lakini hazikutosha kupendekezwa katika nafasi aliyopewa yeye.

## 2.3 SEHEMU C: Maswali ya Insha


Sehemu hii ilikuwa na maswali matatu ya insha (9,10 na 11) kutoka katika mada za Nguzo za *Uislamu, Qur'an na Sunnah na Hadith.* Mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali mawili. Kila swali lilikuwa na alama 15, hivyo, sehemu hii kufanya kuwa kuwa na jumla ya alama 30.

### 2.3.1 Swali la 9: Nguzo za Uislamu

Swali hili lilitoka katika mada ya Nguzo za Uislamu mada ndogo ya Hijja. Katika swali hili mtahiniwa alitakiwa kubainisha changamoto nne zinazosababisha kutoonekana kwa matokeo ya Ibada ya Hijja. Swali

lilipima umahiri wa watahiniwa kutathmini utekelezaji wa ibada ya Hijja katika kufikia malengo yake.


Takwimu zinaonesha kuwa watahiniwa 76,829 (94.82%) kati ya 81,023 (100%) walifanya swali hili. Kati yao, watahiniwa 34,580 (45.01%) walipata alama 9.5 hadi 15 ambao ni ufaulu mzuri. Watahiniwa 23,084 (30.04%) walipata alama 4.5 hadi 9 ambao ni ufaulu wa wastani na watahiniwa 19,165 (24.95%) walipata 0 hadi 4 ambao ni ufaulu dhaifu Chati Na. 9 inaonesha muhtasari wa ufaulu wa watahiniwa hao kwa asilimia.




**Chati Na. 9:** *Asilimia ya Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 9*

Chati Na. 9 inaonesha kuwa ufaulu wa jumla katika swali hili ulikuwa mzuri kwani asilimia 75.05 ya watahiniwa walipata alama 4.5 hadi 15 ikilinganishwa na asilimia 24.95 ya watahiniwa waliopata alama dhaifu (0 hadi 4).

Uchambuzi uliofanyika katika majibu ya watahiniwa umeonesha kuwa, ufaulu mzuri wa watahiniwa uliofikiwa katika swali hili ulichangiwa na maarifa waliyokuwa nayo watahiniwa hao, sambamba na kubaini matakwa ya swali. Watahiniwa hao walibainisha changamoto mbalimbali zinazosababisha kutoonekena kwa matokeo ya Ibada ya Hijja kama vile; (i) *Kuhiji kwa chumo la haramu*, (ii) *Kutotekeleza masharti ya Hijja*, (iii) *Kutokufuata nguzo za Hijja* na (ii) *Kutolijua na kulizingatia lengo la Ibada ya Hijja.* Kielelezo Na. 9.1 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa katika swali hili.



9\. Hijja ni kuenda kuizuru nyumba tukufu ya Muenyezemungu (Al-qaaba) huko makka kwa muislam muenye uwezo. Ibada hii ya hijja waislam wengi huenda Makka kuhiji lakini matokeo yake ya kuwafanya waislam wawe wacha mungu hayaonekani hili ni kutokana na matatizo yafuatayo:-

Kwanza; Kutokulijua lengo la Hijja: Wengi miongoni mwa waislam wanaokwenda Makka kuhiji huenda kuhiji pasi na kulijua lengo la hijja hivyo hii ni sababu moja kubwa inayo pelekea waislam wengi wanaokwenda hijja ila matokeo ya Hijja kutopatikana. hii ni changamoto kubwa sana inayo sababisha matokeo ya hijja kutokuonekana.

Pili; Kuhijji kwa Chumo la Haramu: Dunia yetu ya sasa ni ya watu kuchuma chumo la Haramu kwani makenki mengi katika nchi yetu yanatoa mikopo kwa riba hivyo kutokana na kuwa watu wanachuma chumo la haramu hivyo hupelekea waislam kuenda kuhijji kwa chumo la Haramu. Hii pia ni miongoni mwa sababu kuu zinazopelekea matokeo ya hijja kutokuonekana.

Tatu; Kutokuwa na Elimu juu ya Ibada ya Hijja: Hii pia ni sababu nyengine inayo pelekea Matokeo ya hijja kutokuonekana kwa kundi kubwa la waislam wanaokwenda hijja hana elimu juu ya Ibada ya hijja hivyo kutokana na kuwa waislam wengi wanaokwenda hijja hawana elimu sahihi juu ya Ibada ya hijja hivyo inapelekea matokeo ya Hijja kutokuonekana.

Nne: Kutokuchunga na Kutokuzingatia Masharti ya Hijja; Ibada ya hijja ni Ibada kama Ibada nyengine hivyo kama zilivyo Ibada nyengine kuwa zina masharti yake lakini pia na Ibada hii ya hijja ina masharti yake kwa hivyo wengi wa waislam wanaokwenda Makka kuhijji hawachungi wala hawazingatii masharti ya hijja suala hili linapelekea matokeo ya hijja kutokuonekana.

Yote kwa yote Ibada ya Hijja ni Ibada Muhimu sana kwa jamii ya waislam na ni Ibada ya lazima kwa kila muislam muenye uwezo kuenda kuitekeleza.

Kielelezo Na. 9.1: Sampuli ya Majibu Sahihi ya Mtahiniwa katika Swali la 9


Uchambuzi zaidi uliofanyika katika majibu ya watahiniwa ulibaini kuwa, watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi na kupata ufaulu wa chini katika swali hili, walikosa maarifa ya kutosha kuhusu mada ya Ibada ya Hijja. Wengine walishindwa kubaini matakwa ya swali husika hivyo, walijibu kwa kueleza mambo mengine ambayo hayahusiani na msingi wa swali.

Baadhi ya watahiniwa hao (walioshindwa kujibu kwa usahihi) walitoa hoja mbalimbali kama vile; *Kutokuwa Muislamu wa kweli, Kumshirikisha Mwenyezi Mungu, Kutokuwa na imani thabiti na kutokumaliza Hijja*. Wengine waliandika*; Vigezo, moyo, ufikirio wa Hijja, masafa yake ni marefu*. Pia wapo walioandika*; Kuingia motoni au peponi ni siri yake muumba, kumuomba Allah (S.W) kwa kufanya ibada zake ipasavyo, matokeo ya Ibada ya Hijja mara nyengine huongezeka ama kupunguzika na udhaifu wa watu wa Hijja unapelekea kutokuyapata matokeo kamili.* Majibu ya watahiniwa hao yaliashiria kuwa walikosa maarifa ya kutosha kuhusu ibada ya Hijjah.

Wengine waliandika; *Ukosefu wa fedha, kuendekeza mambo ya starehe na anasa, kuwasaidia ambao kuwa hawana uwezo.* Vilevile, wengine walijibu kuwa; *Ukafiri katika dini ya Kiislamu, Kudai kuwa Hijja hazifati wakati wake, kutoa madai ya uongo, na kutojua misingi ya Hijja.* Hoja hizi hazikubainisha changamoto ya kutoonekana kwa matokeo ya Hijjah bali ziligusa baadhi ya sababu za watu kutotekeleza ibada hiyo. Kwa ujumla watahiniwa hawa walishindwa kuelewa matakwa ya swali.

Kadhalika, baadhi ya watahiniwa walieleza miiko ya Hijja badala ya changamoto zinazosababisha kutoonekana kwa matokeo ya Ibada ya Hijja. Watahiniwa hao walitoa hoja kama vile; *na mawindo, kujipaka manukato, kula nyama ya mnyama aliyewindwa kunyowa, kupanga mipango ya ndoa, kuowa na kuolewa, kujihusisha.*

Kwa ujumla watahiniwa waliokuwa na ufaulu hafifu katika swali hili walishindwa kujenga hoja sahihi kuhusu changamoto zinazosababisha kutoonekena kwa matokeo ya Ibada ya Hijja. Kielelezo namba 9.2 kimeonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hilo kwa usahihi.




Kielelezo Na. 9.2: Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi Katika Swali la 9

Katika kielelezo Na. 9.2 mtahiniwa ameeleza hoja mbalimbali ambazo kwa ujumla wake sio changamoto kubwa zinazosababisha kutofikiwa matokeo ya ibada ya Hijja bali ni mchanganyiko wa vyanzo vya makossa mbalimbali kwa mujibu wa sheria za Kiislamu.

### 2.3.2 Swali la 11: Sunnah na Hadithi.

Swali lilitoka katika mada ndogo ya kukubalika kwa Hadithi, ambapo mtahiniwa alitakiwa kubainisha udhaifu wa hoja tatu za wapinzani wa Hadithi. Swali lilipima umahiri wa watahiniwa kuchambua udhaifu wa hoja za wapinzani wa Hadithi za Mtume (S.A.W).

Takwimu zinaonesha kuwa watahiniwa 28,443 (35.10%) kati ya 81,023 (100%) walifanya swali hili. Kati yao, watahiniwa 27,259 (95.83%) walipata 0 hadi 4 ambao ni ufaulu dhaifu. Watahiniwa 605 (2.13%) walipata alama 4.5 hadi 9 ambao ni ufaulu wa wastani na watahiniwa 486 (2.04%) walipata alama 9.5 hadi 15 ambao ni ufaulu mzuri. Chati Na. 10 inaonesha muhtasari wa ufaulu wa watahiniwa hao kwa asilimia.




**Chati Na. 10:** *Asilimia ya Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 11*


Chati Na. 10 inaonesha kuwa, ufaulu wa jumla katika swali hili ulikuwa dhaifu kwa kuwa asilimia 95.84 walipata 0 hadi 4 ikilinganishwa na asilimia 4.16 waliokuwa na ufaulu mzuri.

Uchambuzi uliofanyika katika majibu ya watahiniwa ulibaini kuwa, ufaulu dhaifu katika swali hili ulisababishwa na kukosekana kwa maarifa ya kutosha kuhusu mada ya Sunna na Hadithi na baadhi ya watahiniwa kushindwa kubaini matakwa ya swali. Miongoni mwa watahiniwa hao walitoa hoja kama vile; *Wapinzani walikataa msingi wa*

*sheria, Hadithi za mtume zilikuwa hazitimii, Hadithi za Mtume Muhammad (S.A.W) zilikuwa zinaandikwa kwenye magome ya miti*. Wengine waliandika; *Hadithi za Mtume Muhammad (S.A.W) kuhifadhiwa kwa Maswahaba, wapinzani wa kikuraysh na wapinzani ya dini tukufu ya Uislamu.* Pia wengine waliandika*; Kufuata Hadithi za Mtume, Hadith kuchambua na kufafanua ujumbe wa Qur'an na wanadai kwamba Hadithi ni stori za uongo.* Hoja hizi zilionesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu kukubalika kwa Hadithi.

Watahiniwa wengine walieleza aina za Hadithi kwa kuzingatia kigezo cha usahihi badala ya kubainisha udhaifu wa hoja za wapinzani wa Hadithi. Watahiniwa hao waliandika; *Hadithi Dhaifu*, *Hadithi Hassan na Hadithi Maudhui.* Wengine walieleza sababu za kutokuwa na uandishi mkubwa wa Hadithi wakati wa Mtume (S.A.W) kama vile; *Kuwepo kwa mtume mwenyewe*, *Mtume (S.A.W) alikuwa akihofia kuwa Maswahaba watachanganya Qur'an na Hadithi na mtume (S.A.W) na Maswahaba walijishughulisha sana katika uhifadhi wa Qur'an.* Kadhalika, wengine walieleza vigezo vya Hadithi Sahihi kwa kuzingatia matini; *Hadithi isipingane na Qur'an, isiwe na maneno ya uongo ndani yake na Hadithi isipingane na hakika ya kihistoria*. Hoja zote hazikujibu swali bali ziliashiria kuwa watahiniwa walishindwa kubaini matakwa ya swali.

Zaidi ya hapo, wapo pia watahiniwa walioeleza umuhimu wa Hadithi badala ya udhaifu wa hoja za wapinzani wa Hadithi. Watahiniwa hao walitoa hoja kama vile; *Hadithi hutumika na Waislamu kama makatazo na mafundisho katika maisha ya kila siku, humfanya mtu awe na mwenendo na tabia njema na humfanya mtu awe na upendo na kupendwa na watu katika jamii yake.* Majibu haya pia yalionesha kushindwa kubaini matakwa ya swali. Kielelezo Na. 10.1 kinaonesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya mtahiniwa katika swali hili.



11. Miongoni mwa upotofu wa waqi katika dini ya
Uislamu ni kukataa nafasi ya hadithi za mtu
me (s.a.w) kama msingi mkuu wa sheria.
Kubainisha udhaifu wa hoja tatu za wapi
nzani wa msingi huo. kama ifuatavyo.
Wapinzani walikataa msingi wa sheria -
kwa sababu walikuwa wanasema kwa hadithi -
za mtume zilikuwa ni ~~badhi~~ hadithi ambazo
zina makosa ndani yake na kupelekea kuka-
taa msingi wa hadithi katika uislamu.
Wapinzani wa msingi huo walikuwa wana
sema hadithi za mtume zilikuwa hazitimia -
katika kukamilisha kwake wakati wakuzi natili
ndomana walikuwa ~~[illegible]~~ ~~kuka~~ wanaka
taa kuwa na hadithi za mtume
Hadithi za mtume zilikuwa hadithi ambazo
~~zina~~ hazina makosa kwa sababu alikuwepo
mtume mwenyewe hatakama wapinzani wali
kuwa wanasema hivyo
Wapinzani wa msingi huo wali wakika-
taa nafasi ya Hadithi za mtume kwa sababu
kama msingi mkuu wa sheria ndomana wapin
zani hawataki kusoma hadithi bali walikuw
a wakiipinga hadithi za mtume na -
kupelekea mtume (s.a.w) kukasirika katika -
hadithi hiyo.
Kwa hiyo udhaifu wa wa hoja -
tatu za wapinzani wa msingi huo walikuw
a hawaipendi hadithi za mtume

Kielelezo Na. 11.1: Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi Katika Swali la 11

Katika kielelezo Na. 11.1 mtahiniwa ameeleza baadhi ya hoja za kubuni ambazo pia hakueleza udhaifu wake, hivyo alishindwa kupata alama katika swali.

Uchambuzi zaidi uliofanyika katika majibu ya watahiniwa ulibaini kuwa, waliopata ufaulu mzuri katika swali hili walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu Sunnah na Hadithi hususani kukubalika kwa Hadithi za Mtume (S.A.W). Watahiniwa hao pia walielewa vema matakwa ya swali hilo na kuweza kueleza kubainisha hoja za wapinzani wa Hadithi na udhaifu wa hoja hizo kama vile; *Hakuna Hadithi sahihi kwa sababu Hadithi hazikufuata mpangilio wa Qur'an katika kuandikwa na kuhifadhiwa. Udhaifu wa hoja hii kutoandikwa kwa Hadithi kama ilivyoandikwa ndani ya Qur'an haibatilishi umuhimu wa Hadithi na wala katazo la Mtume (S.A.W) mwanzoni kuwa Hadithi zisiandikwe haimaanishi kuwa Hadithi si muhimu. Pia udhaifu mwengine wa hoja hii kazi ya Hadithi ni kuitafsiri Qur'an kivitendo, hivyo, kuwepo kwake Mtume (S.A.W) akiwa hai kulitoa fursa kwa maswahaba kujifunza kwa kumuona na kumuuliza moja kwa moja namna ya kuitekeleza Qur'an katika maisha yao.*

*Hadithi zilikusanywa baada ya miaka mingi kupita toka alipokufa Mtume (S.A.W). Udhaifu wa hoja hii ni kwamba, mafundisho ya Mtume (S.A.W) yalihifadhiwa katika vifua na vitendo tokea uhai wa Mtume (S.A.W) na kurithishwa kizazi hadi kizazi baada ya kufariki kwake.*

*Wanadai kuwa ni vigumu kujua maneno halisi ya Mtume (S.A.W) na yale yaliyozushwa na watu kwa ajili ya kutetea upande wao baada ya kuibuka mgogoro baina ya Waislamu na kugawanyika katika makundi. Udhaifu wa hoja hii ni kwamba migogoro na kuzuka kwa Hadithi za uongo lakini walikuwepo maswahaba na wanazuoni wachamungu ambao hawakufungamana na upande wowote. Vilevile, katika juhudi zao za kuhifadhi Hadithi sahihi wanazuoni waliweka vigezo maalumu vya kuchunguza usahihi wa Isnadi na Matini za Hadithi na kuzipa madaraja husika.* Kielelezo Na. 10.2 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa katika swali hili.

11 Hadithi ni masimulizi au mapokezi ya mtume (S.A.W). Katika maisha ya mtume (S.A.W) kuna matendo mbalimbali ambayo aliyafanya na alikuwa nayo na masuala waliomuuliza. Pia hadithi zinasehemu kuu tatu (3) ambazo ni Isnadi, Matini na Rawiliy. Hivyo basi hadithi zinafaida mbali mbali katika jamii. Ila pia kuna watu ~~wa~~ waliokuwa wakisema kuwa hawazikubali hadithi za mtume (S.A.W) waliokuwa wakijuulikana kama ni Al-Qur-anniyuna. Hoja pamoja na udhaifu wa hoja zao walizotaja walikisema ni kwamba;

Hadithi sio sahihi kwa sababu hazikufuata mpangilio wa Qur-an katika kushuka kuteremshwa na kuhifadhiwa; Watu hao walikuwa wakidai kuwa hadithi sio sahihi kwa sababu hazikufuata mpangilio wa Qur-an na **Udhaifu** wa hoja hiyo ni kwamba kutokufuata mpangilio wa Qur-an sio sababu ya kusema hadithi sio sahihi na pia Hadithi ni maelezo juu ya tabia za mtume (S.A.W) na masahaba waliyarithi baada ya kufa kwake.

Hadithi zilikusanywa baada ya miaka mingi kupita toka alipokufa Mtume, Je walijuaje kuwa hizi na hadithi za mtume au ni maneno ya mtume (S.A.W)? ; Pia kuna miaka mingi yalipita toka alipokufa mtume (S.A.W) na ndipo hadithi zikaanzwa kukusanywa lakini pia sio sababu ya kukataa hadithi za mtume (S.A.W). **Udhaifu** wa hoja huyo ni kwamba Vigezo vya isnadi, matini na rawatiy vilitumika katika kutambua usahihi wa hadithi Hivyo vigezo hivyo vilitumiwa ili kusahihisha hadithi

Pia; Baada ya kufa Mtume (S.A.W) waislamu waligawanyika makundi tofauti na kuzusha maneno na kudai ni hadithi za mtume, je mulijuaje kuwa hii ni hadithi sahihi? Vilevile walidai kwa matatabaka yaliyowekwa na waislamu baada ya kufa Mtume (S.A.W) yalizua hadithi tofauti na kudai kuwa ni hadithi za mtume, hivyo basi **Udhaifu** wa hoja hiyo ni kwamba Kulikuwa na wanazuoni mashuhuri walioidhatiti katika kusahihisha hadithi za mtume na pia walizingatia vigezo vya Isnadi, Matini na Rawatiy

Hivyo basi, kuna watu au wapinzani mbalimbali wanaosema kuwa hadithi za Mtume (S.A.W) sio sahihi lakini hoja zao zote zina udhaifu mbalimbali hivyo basi tunapaswa kuwapa elimu watu hao ili waweze kutoka katika upotofu huo

Kielelezo Na. 10.2: Sampuli ya Majibu Sahihi ya Swali la 11

## 3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU KWA KILA MADA

Mtihani wa somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu mwaka 2023 uliundwa na mada kumi na tisa (19). Mada kumi (10) kati ya hizo zilitahiniwa katika swali la kwanza ambalo lilikuwa na vipengele kumi vya kujibu kwa kuchagua. Mada zilizounda vipengele hivyo ni; *Mtazamo wa Uislamu Juu ya Elimu, Imani ya Kiislamu, Mtazamo wa Uislamu Juu ya Dini, Nguzo za Uislamu, Mambo ya Lazima Kufanyiwa Maiti wa Kiislamu, Fiqh, Sunnah na Hadithi, Qur'an, Historia katika Uislamu,* na *Bara Arab zama za Jahiliyyah,* ambapo ufaulu wa jumla katika mada hizo ulikuwa asilimia 89.33.

Kati ya mada hizo zilizotahiniwa katika mtihani huu mada nne zilikuwa na ufaulu mzuri ambazo ni; *Nguzo za Imani* (89.97%) *Mfumo wa Jamii ya Kiislamu* (80.12%), *Nguzo za Uislamu* (77.93%) na *Historia ya Uislamu Baada ya Kutawafu Mtume (S.A.W)* (72.68%), Aidha ufaulu mzuri wa watahiniwa katika mada zilizotajwa ulichangiwa na maarifa ya kutosha waliyokuwanayo, na uwezo waliouonesha katika kubaini matakwa ya maswali na kujibu ipasavyo.

Kwa upande mwingine zilijitokeza mada tatu zilizokuwa na ufaulu wa wastani ambazo ni; *Familia ya Kiislamu* (55.60%), *Haki na Uadilifu katika Uislamu* (51.04%), *Dola ya Kiislamu Madina* (50.29). ufaulu huo ulisababishwa na hali ya watahiniwa kutokuwa na maarifa ya kutosha katika mada husika na wengine kuchanganya baadhi ya hoja sahihi na zisizo sahihi katika majibu waliyotoa. Halikadhalika, watahiniwa wengine kushindwa kufafanua vema hoja sahihi walizotoa katika majibu yao.

Aidha, ufaulu hafifu ulijitokeza katika mada moja ya Sunnah na Hadithi (4.16%). Ambapo, uchambuzi unaonesha kuwa watahiniwa wengi walishindwa kujibu swali kutoka katika mada hiyo kwa sababu ya kukosa maarifa. Wengine walishindwa kubaini matakwa ya swali na hatimae kushindwa kujenga hoja sahihi katika kujibu.

Muhtasari wa ufaulu katika mada zote umeoneshwa katika Kiambatisho cha pekee, ambapo rangi ya kijani imetumika kubainisha mada zilizokuwa na ufaulu mzuri, rangi ya njano imetumika kubainisha mada zilizokuwa na ufaulu wa wastani na mwisho rangi nyekundu imetumika kubainisha mada iliyokuwa na ufaulu hafifu.

## 4.0 HITIMISHO

Kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika Mtihani wa Kuhitimu Kidato cha Nne (CSEE) 2023 somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu kilikuwa kizuri, hii ni kwa sababu asilimia 81.82 ya watahiniwa walipata wastani wa gredi A hadi D ikilinganishwa na asilimia 18.18 ya watahiniwa waliopata gredi F.

Uchambuzi huu umeonesha changamoto mbalimbali zinazopaswa kutatuliwa ili kuboresha zaidi kiwango cha ufaulu katika mitihani ijayo. Changamoto hizo ni kama vile; watahiniwa kukosa maarifa ya kutosha katika mada mbalimbali hususani mada za *Familia ya Kiislamu* (55.60%), *Haki na Uadilifu katika Uislamu* (51.04%), *Dola ya Kiislamu Madina* (50.29) na hasa mada ya *Sunnah na Hadithi* (4.16%).

Kadhalika, kushindwa kubaini matakwa ya maswali na wengine kushindwa kujenga hoja na kuzifafanua ipasavyo (hususani katika maswali ya majibu mafupi). Vile vile, kuchanganya hoja sahihi na zisizo sahihi katika kujibu maswali.

## 5.0 MAPENDEKEZO

Ili kuinua zaidi kiwango cha ufaulu wa somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu katika mitihani ijayo, juhudi zinahitajika katika kuboresha mchakato wa ufundishaji, ujifunzaji na upimaji endelevu wa wanafunzi shuleni. Pamoja na mambo mengine, juhudi hizo zinapaswa kuelekezwa katika kuwaimarisha wanafunzi kimaarifa juu ya mada za somo hususan mada ya Sunnah na Hadithi. Vile vile, kuwajengea wanafunzi uwezo wa kuelewa matakwa ya maswali na kujenga hoja madhubuti katika kujibu. Ili kuweza kufanikisha hayo, yafuatayo yanapendekezwa:

(a) Walimu kuzingatia matumizi ya vitabu vya kiada na mbinu shirikishi katika ufundishaji ili kufikia umahiri uliyokusudiwa katika kila mada.

(b) Walimu kuwapima wanafunzi katika nyanja za juu za kufikiri ili kuimarisha uwezo wao na kuendana na hatimae kwenda sawa na mabadiliko.

(c) Wanafunzi kuzingatia mbinu za kusoma kwa kuelewa ili kuwa na uwezo wa kujenga hoja sahihi na kuzifafanua ipasavyo.

(d) Walimu kuzingatia muhtasari wa somo katika kila hatua ya ufundishaji ili kuepuka na maoni yasiyo rasmi kitaaluma katika somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu.

**Kiambatisho**

## Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa katika Mada CSEE 2023

| Na. | Mada | Ufaulu wa Kila Swali | | Asilimia ya Watahiniwa walio na wastani wa 30 na zaidi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Namba ya Swali | Asilimia ya Ufaulu | | |
| 1 | Nguzo za Imani | 3 | 89.87 | 89.87 | Vizuri |
| 2 | Mtazamo wa Uislamu Juu ya Elimu, Imani ya Kiislamu, Mtazamo wa Uislamu Juu ya Dini, Fiqh, Mambo ya Lazima Kufanyiwa Maiti Muislamu, Bara Arab zama za Jahiliyyah, Historia katika Uislamu, Sunna na Hadithi, Qur'an na Nguzo za Uislamu. | 1 | 89.33 | 89.33 | Vizuri |
| 3 | Mfumo wa Jamii ya Kiislamu | 6 | 80.12 | 80.12 | Vizuri |
| 4 | Nguzo za Uislamu | 2 | 80.80 | 77.93 | Vizuri |
| | | 9 | 75.05 | | |
| 5 | Historia ya Uislamu baada ya Kutawafu Mtume (S.A.W) hadi hivi leo. | 8 | 72.68 | 72.68 | Vizuri |
| 6 | Familia ya Kiislamu | 4 | 55.60 | 55.60 | Wastani |
| 7 | Haki na Uadilifu | 7 | 51.04 | 51.04 | Wastani |
| 8 | Dola ya Kiislamu Madinah | 5 | 50.29 | 50.29 | Wastani |
| 9 | Sunnah na Hadithi | 11 | 4.16 | 4.16 | Dhaifu |
| **Wastani wa Jumla wa Ufaulu katika Mada** | | | | **63.45** | Wastani |